

# MAANDALIZI

# KABLA WAWEKEZAJI

# WATARAJIWA

# HAWAJAFIKA

MWONGOZO  
KWA AJILI YA  
- MAPATANO NA  
WAWEKEZAJI  
KATIKA JAMII

**MWONGOZO 1** Kwa ajili ya wanajamii na watetezi wanaowasiliana na wawekezaji watarajiwa



# MAANDALIZI KABLA WAWEKEZAJI WATARAJIWA HAWAJAFIKA



**Shukrani:** Sehemu ya Mwongozo huu imefadhiliwa na Shirika la UKAid kupitia Idara ya Maendeleo ya Kimataifa, lakini mawazo yaliyomo humu sio lazima yawe yanawakilisha mawazo ya Serikali ya Uingereza.

Mwongozo huu umetokana na msaada wa kitafiti wa Nadeeya Salleh, Netsanet Tesfay, na Lauren Waugh. Tunapenda kuwashukuru hasa Karl Marx Carumba, Sonkita Conteh, Lorenzo Cotula, Leslie Hannay, na Chris Tanner kwa mchango wao mathubuti katika mapitio ya rasimu za awali za mwongozo huu. Tunawashukuru pia Wynston Benda-Henries, David Bledsoe, Lien de Brouckere, Fatmata Fouard-Kanu, Morris Gorwor, Gleadae Harmon Hoskins, John Mwebe, James Otto, Daniel Sesay, Hassan Sesay, Téodyl Nkuintchua Tchoudjen, Abdulai Tommy, na Tom Weerachat kwa mrejesho na ushauri mzuri waliutoa wakati wa uandaaji wa mwongozo huu. Pia tunapenda kumshukuru Sabrina Leroe kwa msaada wake wa uhariri.

Mwisho, tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa watu binafsi waliohudhuria warsha zinazohusiana na Mwongozo huu zilizofanyika nchini Laos, Liberia, Sierra Leone, na Marekani.

**Waandishi:** Rachael Knight, Kaitlin Y. Cordes, Sam Szoke-Burke, na Tehtena Mebratu-Tsegaye, pamoja na Marena Brinkhurst. Mwongozo huu pia umetohoa baadhi ya maelezo kutoka katika Mwongozo ulioandaliwa na Rachel Knight, Marena Brinkhurst na Jaron Vogelsang, "Mwongozo kwa ajili ya Uwezesaji wa Ulinzi wa Ardhi ya Jamii" (Namati, 2016).

**Vielelezo:** © Nnaemeka Ekeocha, simu ya mkononi: +234 8125768790, +234 8034924215, barua pepe: [jornigun@gmail.com](mailto:jornigun@gmail.com)

**Usanifu:** [tania@onehemisphere.se](mailto:tania@onehemisphere.se), simu ya mkononi: +46 732022722, [onehemisphere.se](http://onehemisphere.se)



Kituo cha Uwekezaji Endelevu cha Columbia ni kituo kinachoongoza kwa utafiti unaotumika, na jukwaa lililoundwa kwa ajili ya kujifunza na kujadili uwekezaji endelevu wa kimataifa.

[ccsi.columbia.edu](http://ccsi.columbia.edu)



Namati ni shirika la kimataifa lililoundwa kwa ajili ya kuendeleza nyanja ya uwezesaji wa kisheria na kuimarisha uwezo wa watu wa kudai na kulinda haki zao.

[namati.org](http://namati.org)

## YALIYOMO

UTANGULIZI	4
JINSI KIELELEZI HIKI KILIVYOPANGILIWA	6
FAHARASA YA MANENO	7

### **a** / MAANDALIZI KABLA WAWEKEZAJI WATARAJIWA HAWAJAFIKA

1. Kuelewa kwanini uwekezaji unafanyika na unaweza kuwa na maana gani kwa jamii	10
2. Kufafanua maana ya “jamii,” ili kuhakikisha ushiriki wa wanajamii wote na kuimarisha umoja wa kijamii	11
3. Kuyaona matarajio yajayo ya jamii	14
4. Kuelewa thamani ya ardhi na rasilimali za jamii kwa wanajamii	18
5. Kuhakikisha wanajamii wanaelewa haki zao za ardhi na rasilimali	20
6. Kubaini vipaumbele vya jamii, kusaidia maamuzi ya jamii, na kutunga sheria ndogo ndogo	24

### **b** / MWEKEZAJI ANAPOFIKA KUTAFUTA ARDHI

7. Kuelewa haki ya jamii ya kuhusishwa katika mashauriano	32
8. Kuhakikisha kwamba jamii inahusishwa kikamilifu katika mashauriano	35
9. Kupitia taarifa zote za kisheria, kitaalam na kifedha za kampuni na uwekezaji unaopendekezwa	38
10. Kukamilisha mchakato wa mashauriano: kuamua kukataa uwekezaji unaopendekezwa au kufanya maelewano na mwekezaji	41
11. Kujiandaa kwa ajili ya kuafikiana kuhusu mkataba kati ya jamii na mwekezaji	45
12. Kuanza mashauriano	49



# UTANGULIZI

## NI NINI AZMA YA MIONGOZO HII?

Mwekezaji anaweza kuifikia jamii wakati wowote akihitaji ardhi na rasilimali. Miongozo hii inatoa mapendekezo kuhusu namna ambavyo watetezi na viongozi wa jamii wanaweza kuzisaidia jamii kujiandaa, na endapo zikiamua basi ziingie katika majadiliano ya kina kuhusu mikataba na wawekezaji wanaotaka kutumia ardhi na rasilimali za jamii kwa ajili ya biashara zao.

Mwongozo huu (**Mwongozo 1**) unaeleza namna ambavyo jamii zinaweza kujiandaa kwa majadiliano na wawekezaji watarajiwa, ikiwemo kufanya maamuzi kuhusu kufikia makubaliano au la. Mwongozo unaweza kutumika kuisaidia jamii: (a) kujiandaa *kabla* mwekezaji hajafika (b) kuamua kuingia katika majadiliano au la na mwekezaji ambaye ameshafika. Mwongozo 1 unapaswa utumike *kabla* ya kuanza maafikiano yoyote.

Endapo jamii itaamua kuafikiana na mwekezaji mtarajiwa, **Mwongozo 2** unaeleza mambo ambayo yanaweza kuingizwa ndani ya mkataba kati ya jamii na mwekezaji. Mwongozo huu unaeleza pia lugha ipi iepukwe. Umeandaliwa kuzisaidia jamii kuafikiana na kupata mkataba ulio wazi, unaozingatia haki na usawa.

## MIONGOZO HII NI KWA AJILI YA NANI?

Miongozo hii inalenga makundi mawili makuu:

- ➔ Wanasheria, wasaidizi wa kisheria, watetezi, wahamasishaji, na wataalamu wengine wanaoisaidia jamii katika masuala ya kisheria yanayohusu usimamizi na ulinzi wa haki za binadamu, ardhi yao, rasilimali zao (watu ambao Miongozo hii inawaita “**watetezi**”);
- ➔ Viongozi wa jamii na wanajamii wanaotafuta taarifa kusaidia majadiliano yao na wawekezaji watarajiwa na ambao wanafanya kazi pamoja na wanasheria, wasaidizi wa kisheria, na watetezi wengine. **Hata hivyo, jamii hazipaswi kuutumia Mwongozo huu kama mbadala wa msaada wa kisheria.**

Pamoja na kwamba makundi haya ndio makundi lengwa ya Miongozo hii, **watetezi na viongozi hawapaswi kufanya mashauriano na kufanya maamuzi yanayohusu uwekezaji peke yao.** Baadala yake, wanapaswa kuhakikisha ushiriki wenye tija katika kila uamuzi unaohusu uwekezaji wa wanajamii, wakiwemo wanawake, vijana, watu wenye mikakati tofauti ya kujikimu, na watu kutoka katika makundi ya watu wachache waliosahaulika.

## KWANINI MIONGOZO HIII INAHITAJIKA?

**Kuamua kumruhusu mwekezaji atumie ardhi na rasilimali ya jamii au la, ni moja ya maamuzi muhimu ambayo jamii inaweza kuyafanya. Mradi wa uwekezaji unapotekelezwa kwa namna ambayo inaheshimu na kuhusisha wahusika wote wakuu, unaweza kuwasaidia wanajamii kufikia malengo yao.** Malengo hayo yanaweza kuwa ni pamoja na kutengeneza ajira na fursa za kiuchumi. Lakini uwekezaji unakuja na athari zake. Miradi ya uwekezaji inaweza kuifanya ardhi ambayo wanajamii wanaihitaji kwa kilimo na shughuli nyingine za kujikimu isiweze kutumika kwa muda fulani. Inaweza kuchafua mito, maziwa, hewa na udongo. Inaweza kuzuia ufikiwaji wa baadhi ya maeneo muhimu na vyanzo vya maji. Inaweza hata kukiuka haki za binadamu za wanajamii. Wakati mwingine, miradi ya uwekezaji inaweza kupelekea jamii zipoteze kabisa ardhi yao.

**Huenda inawezekana kupunguza hatari zinazohusiana na uwekezaji iwapo jamii zinafahamu haki zake; zinaelewa faida na hasara, na hatari zitokanazo na uwekezaji; na zinasimamiwa na watetezi wanaowasaidia wanajamii kulinda maslahi yao.** Kuziandaa jamii kujadiliana na wawekezaji watarajiwa kutoka katika nafasi ya uwezeshaji, kunaweza kuboresha maafikiano ya kimkataba na kuhakikisha kwamba uwekezaji unachangia maisha ya baadae yaliyoshamiri na yenye manufaa ya jamii husika. Jamii iliyowezeshwa inaweza kudai wawekezaji waheshimu matakwa ya jamii, walinde mazingira ya mahali husika, na kutoa msaada kwa ajili ya maendeleo ya jamii, kwa kufuata masharti ya jamii yenyewe.



**Miongozo hii haitoi ushauri wa kisheria na haigusii masuala yote muhimu ya kisheria. Endapo jamii itaamua kuafikiana na mwekezaji, ni vyema iwe na wakili wake binafsi ambaye ataupitia mkataba kabla jamii haijatia saini.**

## MUKTADHA WA MIONGOZO HII

Hivi leo, duniani kote, kuna ushindani juu ya ardhi na rasilimali ambazo zinazidi kupungua. Kwa muktadha huu, wanajamii wanapaswa kujiandaa kujadiliana na wawekezaji watarajiwa wanaotafuta ardhi na rasilimali. Wawekezaji hawa wanaweza kutoka katika jamii husika au kutoka katika tabaka la watu wenye nafasi nzuri nchini, maafisa wa serikali, au wawekezaji wa kimataifa. Wanaweza wakaomba hekari chache tu, au *maelfu* ya hekari. Zipo “nyakati” tatu ambazo jamii zinaweza kupitia katika muktadha huu, na kila moja inahitaji ujuzi na maarifa tofauti:

1. **Kabla mwekezaji hajafika**, jamii zinapaswa kuhakikisha kwamba ardhi yao na maliasili zao ziko salama na zinalindwa, na kwamba zinasimamiwa na sheria na miundo thabiti. Bila kuwa na haki thabiti juu ya ardhi, jamii zinaweza kushindwa kulinda ardhi yake kutoka kwa wawekezaji wa nje na matokeo yake jamii hizi zitakuwa katika nafasi dhaifu ya kufikia maafikiano na wawekezaji watakapofika. Usimamizi wa ardhi ya jamii ambao ni shirikishi na wajibishi unaweza kusaidia kuhakikisha kwamba mikataba yoyote ya siku za mbele kati ya jamii na mwekezaji inanufaisha siyo tu viongozi wa jamii na tabaka la watu wenye uwezo (wenye nafasi nzuri) katika jamii, bali pia wanawake, vijana, familia maskini, na watu kutoka katika makundi yaliyosahaulika na yenye watu wachache.
2. **Kipindi ambacho mwekezaji mtarajiwa anafika kwa mara ya kwanza kutafuta ardhi na rasilimali**, mwekezaji huyo anaweza pia akawa anaiomba serikali kibali cha kuendesha mradi wake wa biashara. Katika nchi nyingi, wawekezaji ni lazima waombe na wapate leseni ya mazingira, leseni ya biashara, na aina nyingine za vibali (idhini) kutoka serikalini. Michakato hii ya kupata vibali vya serikali inaweza kujenga fursa kwa jamii kushawishi masharti ambayo serikali itatoa kuhusu uwekezaji husika. Kwa mfano, jamii inaweza kuiomba serikali idai ulinzi madhubuti wa mazingira kabla haijatoa kibali kwa mwekezaji.
3. **Baada ya mwekezaji kupewa haki ya kutumia ardhi ya jamii na ameanza shughuli za mradi**, wanajamii wanapaswa kufuatilia uwekezaji huo na athari zake kwa jamii. Wanapaswa pia kufuatilia kuona kama mwekezaji anatii masharti ya mkataba na sheria za nchi au la. Matatizo yanapotokea, wanajamii wanaweza kupeleka malalamiko yao moja kwa moja kwa mwekezaji na/au kupitia michakato ya kiserikali ya kuwasilisha malalamiko na taratibu za kushughulikia madai. Endapo mwekezaji atakataa kushughulikia matatizo hayo, wanajamii wanaweza kutafuta msaada kutoka katika ofisi za serikali au mahakama za eneo husika na kumshinikiza mwekezaji kupitia kampeni za utetezi.

## UTANGULIZI

/ INAENDELEA

“Nyakati” hizi tatu ni fursa muhimu kwa jamii kulinda maslahi yake. Jamii zinapaswa pia kufanya kazi na watetezi **kuimarisha ulinzi wa kitaifa wa sheria zinazohusu haki za ardhi na rasilimali za jamii** kwa ujumla, na katika muktadha wa uwekezaji. Sheria na sera zikiboreshwa zinaweza kulinda vizuri zaidi haki za jamii za muda mrefu.

### SHERIA YA NCHI NI MUHIMU

**Kila nchi inazo sheria mahususi zinazohusu uwekezaji na haki za ardhi ya jamii. Watetezi wanaosaidia au wanaowakilisha jamii ni lazima wafanye utafiti wa sheria za nchi zinazohusika pamoja na kutumia mwongozo huu.** Sheria husika za nchi zinajumuisha sheria zinazotumika kwa ajili ya mikataba, uwekezaji, haki za ardhi, haki za wenyeji, ulinzi wa mazingira, na aina mahususi za miradi.

## JINSI MWONGOZO HUU ULIVYOPANGILIWA

Nusu ya kwanza ya Mwongozo huu inaeleza jinsi ambavyo jamii zinaweza kujiandaa na kujipanga kwa ajili ya wawekezaji watarajiwa. Unaeleza uwekezaji unaweza kuwa na maana gani kwa jamii, jinsi ya kuwasaidia wanajamii kuainisha dira ya pamoja ya jamii yao iliyoshamiri, jinsi ya kuelewa thamani ya ardhi yao kwao, jinsi ya kutunga sheria kuhusu jinsi ya kusimamia ardhi na rasilimali zao, jinsi maamuzi kuhusu ardhi yao yanaweza kufanyika (na nani), na jinsi ya kuhakikisha michakato ya kufanya maamuzi kuhusu wawekezaji watarajiwa ambayo ni shirikishi, inayozingatia haki na ambayo ni jumuishi.



**Iwapo mwekezaji amekwishafika na maamuzi ya haraka yanahitajika, majadiliano haya yanaweza kufanyika kwa haraka zaidi, ndani ya wiki moja.** Hata hivyo, hii haishauriwi: jamii haipaswi kuharakishwa kufanya maamuzi muhimu kama hayo. Jamii inapaswa kuomba muda wa kutosha kufanya utafiti wa kina kuhusu mwekezaji na uwekezaji unaopendekezwa, kuelewa haki za kisheria za jamii, na kuamua kwa uangalifu ni nini kitakuwa na manufaa zaidi kwa jamii.

Nusu ya pili ya Mwongozo huu inaeleza hatua ambazo jamii zinaweza kuchukua baada ya kufuatwa na mwekezaji. Unaeleza jinsi mchakato wa “kushauriana na jamii” unavyopaswa kuendeshwa na hatua mahususi ambazo wanajamii wanaweza kuchukua wanapofanya maamuzi kuanza mashauriano na mwekezaji au kukataa uwekezaji unaopendekezwa.

# FAHARASA YA MANENO

**Faida au hasara za mwaka:** Kiasi cha fedha ambacho kampuni inazalisha au kupoteza, baada ya kutoa gharama, kwa mwaka mzima. Maelezo yanaweza kutolewa kwenye ripoti ya fedha.

**Kipengele:** Sehemu au ibara katika mkataba.

**Jamii:** Kikundi cha watu, familia, na kaya ambacho kwa pamoja kinaishi katika sehemu moja au kina mahusiano ya kihistoria na eneo mahususi lenye mipaka inayofahamika na ambacho kinaongozwa na mifumo ya kitaifa au utawala wa kimila.

**Kampuni:** Chombo kinachojihusisha na biashara. Mwongozo huu unahusika na makampuni na wawekezaji ambao wanaendesha miradi inayotumia rasilimali—hususan miradi ya kilimo au misitu—lakini unaweza pia kuhusika na kampuni zinazojishughulisha na miradi ya uchimbaji wa madini. Neno “Kampuni” na “Mwekezaji” yanatumika kwa kubadilishana katika mwongozo huu. Tazama pia fasili ya neno “Mwekezaji.”

**Mkataba:** Pale ambapo pande mbili au zaidi (watu, jamii, au mashirika) zinapoahidi kufanya jambo fulani ili kupata faida yenye thamani, hii inaweza kuwa kwa njia ya mkataba, ambao “**unawafunga kisheria.**” Pande hizi zinazolingia kwenye mkataba zina haki na wajibu chini ya mkataba huo. Kwa kawaida, hatua au mchakato unaopaswa kufuatwa ili mkataba uwe halali zimeelezwa katika sheria za nchi. Mikataba ambayo ni halali inaunda “**haki za kisheria ambazo zinatekelezeka.**”

**Eneo la mkataba:** Eneo la ardhi ambalo linalindwa na mkataba. Shughuli za kibiashara zinaweza kufanyika katika ardhi hii.

**Mkataba kati ya jamii na mwekezaji:** Mkataba ambao jamii inaingia na kampuni au mwekezaji ambao wanakubliana kuhusu masharti ambayo kampuni inaweza kutumia ardhi na rasilimali za jamii.

**Haki za kisheria zinazotekelezeka:** Haki ambazo zinatambuliwa na kulindwa kisheria. Katika baadhi ya maeneo, haki za kisheria zinazotekelezeka zinajumuisha haki za kimila ambazo zinatokana na sheria za kimila. Haki za kisheria zinazotekelezeka zinaweza pia kuundwa kupitia mkataba. Pande zote zinazohusika na mkataba ni lazima ziheshimu haki hizi za kisheria. Endapo pande moja haitaheshimu haki hizi, inaweza kuamrisha ifanye hivyo na mahakama.

**Tathmini ya athari za kimazingira (EIA):** Utafiti unaotabiri athari za kimazingira zinazoweza kutokana na shughuli za mradi. Tathmini ya athari za kimazingira inaweza kuwasilishwa kama ripoti ambayo lazima ithibitishwe na serikali.

**Uhuru wa kuomba taarifa:** Maombi rasmi kwa serikali ya kupata taarifa ambazo ziko mikononi mwa serikali. Maombi haya yanafanyika kwa mujibu wa sheria za nchi za uhuru wa kuomba taarifa.

**Utaratibu wa kushughulikia madai:** Mchakato kwa ajili ya wanajamii mmoja mmoja kuwasiliana na kutafuta suluhisho la malalamiko na madai kuhusu athari hasi za mradi au mwenendo wa kampuni au wafanyakazi wake.

**Tathmini ya athari za haki za binadamu:** Utafiti ambao unachambua athari zinazoweza kutokea au athari halisi za haki za binadamu za mradi na kutoa mapendekezo ya kushughulikia athari hizo.

**Miundombinu:** Majengo na mifumo inayohitajika kwa ajili ya kuendesha biashara, jiji, au kijiji, kama vile barabara, bomba za maji au visima, Minara ya mawasiliano, na mifumo ya umeme. Miundombinu ya kijamii na mifumo inayotumika kwa ajili ya huduma za jamii, kama vile shule na vituo vya afya.

**Shughuli za uwekezaji:** Shughuli ambazo zinaendeshwa kwa ajili ya mradi wa uwekezaji kwa nia ya kutengeneza faida.



# FAHARASA YA MANENO

/ INAENDELEA

**Mradi wa uwekezaji:** Mradi unaoendeshwa na kampuni au mwekezaji kwa nia ya kutengeneza faida.

**Mwekezaji:** Mtu au chombo kinachoweka fedha katika biashara au miradi ya uwekezaji. Mwongozo huu unahusika na wawekezaji wanaoendesha miradi inayotumia rasilimali—hususan miradi ya kilimo na misitu— lakini wanaweza pia kuwa wawekezaji wanaoendesha miradi ya uchimbaji wa madini. Maneno “Kampuni” na “Mwekezaji” yanatumika kwa kubadilishana katika mwongozo huu. Tazama pia fasili ya neno “mwekezaji.”

**Mkataba:** Mkataba ambao pande moja inahamisha ardhi au mali kwa pande nyingine, au matumizi ya ardhi na mali hiyo, kwa kipindi cha muda maalum, ili kupata malipo kila baada ya muda fulani yanayojulikana kama “kodi.”

**Leseni:** Ruhusa, inayotolewa na serikali, kwa ajili ya kuendesha shughuli maalum. Inafanana sana na “Kibali.”

**Ufuatiliaji:** Kukagua mara kwa mara kuona jinsi mradi unavyofanya kazi na athari zake chanya au hasi. Hii inaweza kufanyika kuona kama kampuni inafuata sheria au mkataba kati ya jamii na mwekezaji. Ufuatiliaji unaweza kuhusisha aina tofauti za utafiti, ikiwemo kupima maji au udongo kuona kama vimechafuliwa, kuhoji wanajamii kuhusu uzoefu wao, au kukagua makaratasi ya kampuni kuhakikisha kwamba kampuni inafuata majukumu yake, kama vile kugawana mapato. Ufuatiliaji unaweza kufanywa na serikali, jamii, kampuni au watendaji wengine.

**Majadiliano kwa ajili ya kuafikiana:** Majadiliano kwa ajili ya kuafikiana yanahusisha watu wawili au zaidi au pande ambazo zinakaa pamoja kwa lengo la kufikia makubaliano. Kila upande unaeleza matakwa yake ambayo yanajadiliwa hadi muafaka unapatikana.

**Pande:** Mtu, jamii, au shirika ambalo linaingia katika mkataba na watu wengine au mashirika.

**Kibali:** Ruhusa, kwa kawaida inayotolewa na serikali, kwa ajili ya kuendesha shughuli maalum. Inafanana sana na “Leseni.”

**Ugawanaji wa faida:** Mwongozo huu, ni makubaliano ambayo jamii inapokea moja kwa moja sehemu ya faida za kampuni kutokana na mradi. Faida ni fedha ambazo kampuni inatengeneza kutokana na mradi baada ya kutoa gharama ambazo kampuni imetumia kuendesha mradi.

**Mrabaha:** Katika Mwongozo huu, mrabaha ni malipo yanayolipwa kwa jamii ambayo yanatokana na kiasi cha bidhaa zilizozalishwa na mradi wa kampuni. Malipo haya yanaweza yakawa asilimia ya thamani ya bidhaa zilizozalishwa (kwa mfano, asilimia 10% ya thamani ya bidhaa zilizozalishwa), au yanaweza kuwa malipo kwa kila sehemu ya bidhaa iliyozalishwa (kwa mfano, Dola 10 za Kimarekani (\$10) kwa kila tani ya bidhaa iliyozalishwa).

**Tathmini ya athari za kijamii:** Utafiti unaochambua athari za kijamii zinazoweza kutokea na athari halisi za mradi, na ambao unapendekeza hatua za kuchukua kukabiliana na athari hizo.

**Kampuni tanzu:** Kampuni ambayo inamilikiwa na kudhibitiwa (sehemu au yote) na kampuni nyingine. Kwa mfano, kampuni inayomilikiwa na taifa zaidi ya moja inaweza kuanzisha au kusajili kampuni tanzu katika nchi ambayo mradi utatekelezwa, ili kampuni hiyo tanzu ipate haki na kutimiza majukumu yote yanayohusiana na mradi.

**Kura ya juu:** Kura ambayo theluthi mbili (66%) ya wapiga kura wanakubaliana na maamuzi yaliyofanyika (tofauti na kura ya jumla, ambayo maamuzi yanaweza kufanyika kwa asilimia 51% tu ya kura za ndiyo).

**Umiliki wa haki:** Haki za kimila au haki rasmi za kisheria kwa ardhi na rasilimali zilizopo katika ardhi hiyo.

**Muda:** Ni kipindi ambacho mkataba unatambulika (uko hai). Wakati mwingine kipindi hiki kinaitwa “muda” wa mkataba.



# a

## MAANDALIZI KABLA WAWEKEZAJI WATARAJIWA HAWAJAFIKA

- |    |   |    |
|----|---|----|
| 1. | Kuelewa kwanini uwekezaji unafanyika na unaweza kuwa na maana gani kwa jamii                    | 10 |
| 2. | Kueleza maana ya “jamii” kuhakikisha ushiriki wa wanajamii wote, na kuimarisha umoja wa kijamii | 11 |
| 3. | Kuuona wakati ujao unaotarajiwa na jamii  | 14 |
| 4. | Kuelewa thamani ya ardhi na rasilimali za jamii kwa wanajamii                                   | 18 |
| 5. | Kuhakikisha uelewa wa wanajamii kuhusu haki zao juu ya ardhi na rasilimali                      | 20 |
| 6. | Kubaini vipaumbele vya jamii, kusaidia maamuzi ya jamii na kutunga sheria ndogo ndogo           | 24 |



# 1.

## KUELEWA KWANINI UWEKEZAJI UNAFANYIKA NA UNaweza KUWA NA MAANA GANI KWA JAMII

Hivi leo, wapo watu wengi zaidi wanaoishi juu ya ardhi, na wengi zaidi wanadai rasilimali ambazo wanahitaji ili kuishi, vikiwemo ardhi, maji, chakula, vifaa vya kujengea, mafuta, na madini yanayohitajika kwa ajili ya teknolojia. Matokeo yake, mashindano ya kupata rasilimali hizi yanaongezeka, na makampuni, serikali na watu wenye uelewa na nafasi nzuri katika jamii wanakimbilia kudai na kuvuna hizi rasilimali.

Inasaidia jamii zikielewa kwa kina kwanini uwekezaji, matumizi/ manunuzi ya ardhi kwa kubuni thamani yake, na unyakuzi wa ardhi vinafanyika katika eneo lao ili iweze kuitikia maombi ya ardhi na rasilimali zao kwa ajili ya miradi yenye tija. Watetezi wanaweza kuwasaidia wanajamii kukaa pamoja na kujadili maswali kama:

- Tuna rasilimali zipi ambazo wawekezaji wanaweza kuzitaka? Ni kwanini ghafla wawekezaji wanaonesha shauku ya kuitaka ardhi yetu?
- Ni nini kimebadilika siku za karibuni katika nchi yetu ambacho kimefanya eneo letu liwavutie wawekezaji wanaotafuta ardhi na rasilimali?
- Ni nini kimebadilika, katika ngazi ya taifa au kanda, ambacho kinafanya ardhi yetu ya jamii iwe hatarini kunyakuliwa?

- Je, kuna miradi yoyote mipya ya miundombinu ya serikali inayopangwa kwa ajili ya eneo letu? Je, kuna bandari mpya, barabara, uwanja wa ndege, au bomba la mafuta ambavyo vinajengwa?
- Je, mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya, mkoa au jimbo limeigawa jamii yetu kwa ajili ya uwekezaji au miradi ya miundombinu ya serikali ya siku za usoni?
- Kumekuwa na mabadiliko yoyote katika siasa za nchi ambayo yameifungua nchi kwa ajili ya uwekezaji wa nje?
- Je, nchi yetu imeibuka kutoka kwenye vita vya wenyewe kwa wenyewe, na sasa wawekezaji wa nje wanajaribu kuchimba rasilimali zenye thamani ambazo zilisahaulika kutokana na ukatili na kuyumba kwa hali ya kisiasa?

Uchambuzi yakinifu wa mienendo hii –na jinsi itakavyoathiri jamii— itawasaidia wanajamii na watetezi wao kujiandaa vizuri zaidi kwa ajili ya kushughulikia maombi ya ardhi na rasilimali za jamii kutoka kwa wawekezaji.





# KUELEZA MAANA YA “JAMII,” KUHAKIKISHA USHIRIKI WA WANAJAMII WOTE NA KUIMARISHA UMOJA WA KIJAMII

## “JAMII” NI NINI, NA NI NANI ANATAMBULIWA KAMA “MWANAJAMII”?

“Jamii” inaweza kufasiliwa kwa ujumla kama *“kikundi cha watu, familia, na kaya ambacho kinaishi pamoja, au kina mahusiano ya kihistoria na eneo mahususi lenye mipaka inayojulikana, na ambacho kinasimamiwa na miundo ya utawala wa kitaifa au kimila.”* Kila jamii inapaswa kujibainisha yenyewe, kwa kufanya marejeo ya kiutamaduni, kisiasa, na kieneo, pamoja na ya matakwa ya wanajamii.

Siyo rahisi wakati wote kubaini nani ni sehemu ya “jamii” na hivyo anapaswa kuhusika katika majadiliano na maamuzi kuhusu matumizi ya ardhi na maliasili. Pale inapowezekana, ni vyema kuzisaidia jamii kujibainisha zenyewe kwa kuzingatia:

- Eneo la ardhi inayomilikiwa, mipaka ya eneo au matumizi ya kushirikiana, na haki za kuitumia eneo;
- Miundo ya utawala wa kimila iliyopo (kijiji, kata, mji, n.k.) inayohusiana na eneo mahususi la ardhi;
- Vigezo vingine vyovyote ambavyo wanajamii wanaona ni muhimu.

Mara nyingi, mipaka iliyopo ya ardhi inayomilikiwa, haki za matumizi, na miundo ya utawala wa eneo, hubadilika kutoka kizazi kimoja kwenda kizazi kingine ili kuendana na muktadha wa kijamii na kimazingira wa eneo husika. Ilimradi tafsiri hizo hazisababishi utengwaji, ubaguzi, au ukosefu wa usawa, kutumia miundo inayokubalika ya eneo husika kutarahisisha uitaji wa mikutano, ukusanyaji watu pamoja, na ufanyaji wa maamuzi ambayo wanajamii wote wataikubali.

Ili kuhakikisha kwamba mipaka ya jamii na uanajamii vinabainishwa vyema, ni muhimu kwamba mchakato wa kuelezea jamii **uhusishe viongozi na watu katika jamii za jirani ambao wamekuwa na matumizi ya kihistoria na haki za matumizi juu ya ardhi husika**, wakiwemo wafugaji na jamii zinazohama hama ambazo

familia zao zimetumia ardhi hiyo kwa muda mrefu. Huenda ikawa sawa kwa watu ambao hawaishi au kujipatia riziki kutoka katika “eneo” husika, lakini wanaweza kuathirika wasipoweza kuitumia ardhi hiyo wachukuliwe kama wanajamii na wahusishwe katika kuamua kama uwekezaji unaotarajiwa ukubaliwe au ukataliwe.

Mara tu mipaka ya jamii ya kieneo inapobainishwa, **kila mtu anaeishi ndani ya “eneo” la jamii lililobainishwa au mwenye haki halali ya matumizi ya kihistoria achukuliwe kama mwanajamii**, mwenye mawazo, dukuduku na maoni muhimu. **Hii inajumuisha wanawake, vijana, watu wenye shughuli mbalimbali za kujikimu, na watu kutoka katika vikundi vyenye watu wachache na waliosahaulika.** Katika baadhi ya maeneo, mipaka ya eneo husika ya nani ni “mwanajamii” imekuwa ikitenga na kubagua; jamii zinapaswa kujadili kwa uwazi kwanini mipaka hii inakuwepo, athari za mipaka hii, na jinsi ya kupunguza ubaguzi ili kuhakikisha haki halali za kila mtu za kutumia na kufikia ardhi ya eneo husika hazikiukwi.

Katika baadhi ya maeneo, **mwekezaji anapokuja kutafuta ardhi ambayo inahusisha vijiji au miji kadhaa, maana ya “jamii” inaweza kupanuliwa ili ijumuishe eneo la jumla la ardhi inayoombwa na mwekezaji.** Hii inaweza kutokea hata kama kwa kawaida watu wanaoishi katika kila kijiji au mji wanajiona kama wanatoka katika “jamii” tofauti. Katika hali kama hizi, vijiji vyote vinaweza kufaidika kwa kujikusanya pamoja kama “jamii” moja na kufanya maamuzi ya pamoja. Au, kama vijiji hivi tofauti vinataka kubaki kama “jamii” tofauti, wawakilishi kutoka katika kila jamii wanaweza kukutana kama kikundi kujadili mipango yao lakini wakashauriana na mwekezaji wao wenyewe kwa niaba ya vijiji au miji yao mahususi, ambavyo huenda vikawa na masilahi, matakwa, na mahitaji tofauti.

## KUHAKIKISHA USHIRIKI WA WANAJAMII WOTE

Ufanyaji maamuzi kuhusu uwekezaji unapaswa uwe wa wazi na ujumuishe ushiriki wa kila mwanajamii. Viongozi hawapaswi kufanya maamuzi pekee yao. Baadala yake, wanajamii wote— wakiwemo wanawake, vijana, wazee, wanajamii walio na hali duni zaidi, watu wanaojipatia riziki kutokana na shughuli mbalimbali, watumiaji wa muda, na watu wanaotoka katika makabila au vikundi vyenye watu wachache wapaswa kupata fursa ya kushiriki katika utoaji wa maamuzi kuhusu matumizi na usimamizi wa ardhi na na rasilimali za jamii ambavyo vinaweza kuathiri ustawi wao kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Ili kuhakikisha kwamba vikundi ambavyo kwa kawaida vinatengwa kutoka katika majadiliano yanayohusu ardhi ya jamii, jamii zinaweza kufanya yafuatayo:

- Kuandaa mfumo wa uhamasishaji ambao unajumuisha wahamasishaji wanawake na vijana ili wahamasishe vijana wa mahali husika na wahamasishaji wa watu kutoka kwenye makabila au dini zenye wafuasi wachache kuhakikisha kwamba watu kutoka katika makundi hayo wanahudhuria mikutano yote muhimu katika jamii;
- Kupanga mikutano muda ambao wanawake, vijana na watu kutoka katika vikundi vya watu wachache hawana shughuli nyingine za kazi na

kufanya mikutano mahali ambapo panaweza kufikika na vikundi vyote;

- Kuendeleza kusisitiza umuhimu wa kujumuisha sauti za watu wote katika majadiliano na kukubaliana kuhusu kanuni wakati wa mikutano ya jamii ambazo zinahakikisha kwamba wawakilishi wa makundi yote wanaweza kushirikishana mawazo na maoni yao; na
- Kuandaa mikutano tofauti kwa ajili ya wanaume, wanawake, vijana, na vikundi vingine ili kuhakikisha kwamba sauti za watu wote zinasikika (kwa mfano, wanawake wanaweza wasijisikie huru kuzungumza mbele ya wanaume lakini wakazungumza kwa uhuru katika mkutano wa wanawake tupu). Baada ya kukutana katika makundi tofauti, vikundi hivi vinaweza kukutana tena pamoja kutoa taarifa ya pamoja na kujadili mawazo na dukuduku zao.

Mashauriano katika jamii yanapaswa kumhusisha kila mtu mwenye makazi ya kudumu na anaefanya shughuli ndani ya eneo husika kijiografia pamoja na watu wanaotumia ardhi na rasilimali ya jamii kwa muda ambao wana haki ya kihistoria ya kufanya hivyo.

Unganeni kama jamii: kijiti kimoja kinaweza kuvunjika kirahisi, lakini si rahisi kuvunja fungu la vijiti.





## KUIMARISHA UMOJA WA KIJAMII

Mshikamano wa kijamii—ile hali ya kuwa pamoja na kuwa na maadili sawa miongoni mwa wanajamii—ni muhimu kwa ajili ya utoaji wa maamuzi ya amani na ushirikiano kuhusu ardhi na rasilimali. Hata hivyo, jamii sio za jinsi moja—jamii yenye watu 300 inaweza kuwa na mitizamo na matakwa zaidi ya 300 tofauti! Mwekezaji mtarajiwa anapofika, hata jamii zenye umoja zinaweza kugawanyika. Bila umoja wa kijamii, inakuwa vigumu zaidi kwa wanajamii kufikia makubaliano kuhusu kumruhusu au kutomruhusu mwekezaji atumie ardhi na rasilimali za kijiji.

Jamii inapojihisi kwamba ni kikundi kilichoshikamana, maamuzi kuhusu matumizi ya ardhi ya jamii yanaweza kuwa na mafanikio zaidi. Umoja pia unasaidia kuzuia wawekezaji kuigawa jamii, hususan kama mwekezaji anafanya vitendo vya makusudi kujaribu kusababisha au kuchochea hali ya kutoelewana ili aweze “kuigawa na kuiteka” jamii.

**Jamii inaweza kutaka kujadiliana kabla ya muda kuhusu jinsi wanajamii watakvoyohakikisha kwamba mbinu zozote za “kugawa na kuteka” zinazotumika na wawekezaji watarajiwa hazifanikiwi.** Wanajamii wanaweza kuulizana: “Tunaweza kufanya nini kuhakikisha watu kutoka nje hawawezi kugawa maoni ya jamii na kujenga ugomvi kati yetu?” Wanajamii wanaweza kutafakari mikakati mbalimbali ya kuwaweka pamoja wakati wa mashauriano na wawekezaji watarajiwa, na wanaweza kukubaliana kuhusu namna ya kushughulikia maoni yanayokinzana. Kwa mfano, jamii zinaweza kuunda sheria ambazo:

- Zinakataza kiongozi wa jamii au kikundi kidogo cha wanajamii kukutana na wawekezaji pekee yao/bila jamii yote kuwepo, au
- Zinakataza viongozi kufanya maamuzi kuhusu ardhi na rasilimali za jamii bila kushauriana na wanajamii wote na kufanya maamuzi kama kikundi kwa kutumia wingi wa kura au kura ya muafaka.

Vile vile, wanajamii wanaweza kukiomba kila kikundi cha wadau watoe maelezo ya sababu ambazo zingewafanya wakubali au wakatae ombi la mwekezaji ili kuweka maoni yote “hadharani” kabla mwekezaji hajafika, katika kipindi ambacho jamii inao muda wa kuelewa vizuri maoni yote moja moja na kutafuta maafikiano na ufumbuzi kuhusu jinsi ya kushughulikia madukuduku na mahitaji ya kila kikundi. Inaweza pia kusaidia kuwa na shughuli ambazo zinajenga ushirikiano, utu, na fahari, kama vile sherehe na hafla za kimila.



- Je, mmekwishakubaliana, kati yenu pamoja na majirani zenu, kuhusu mipaka ya jamii yenu? Mnayo ramani (hata ramani ya kuchora) ya mipaka ya jamii yenu?
- Ni nani ameingizwa kwenye mipaka yenu ya “mwanajamii?” Nani ameachwa? Je, watu wote wenye haki halali, ya kihistoria ya kutumia na kuingia kwenye ardhi wameingizwa katika mipaka hii?
- Mtahakikishaje kwamba sauti za wanajamii wote—wakiwemo wanawake, vijana, watu kutoka katika vikundi vya watu wachache—zinasikika katika utoaji wa maamuzi kuhusu ardhi na rasilimali?
- Mtafanya nini iwapo mwekezaji au mawakala wake watajaribu kukutana na viongozi pekee yao kutafuta haki ya kutumia ardhi na rasilimali za jamii, au wakijaribu kugawa maoni ya jamii kuhusu uwekezaji wa siku zijazo?

### 3.

## KUYAONA MATARAJIO YAJAYO YA JAMII

Wanajamii wanakuwa wamejiandaa vyema zaidi kufanya maamuzi kuhusu – na kuafikiana na – wawekezaji watarajiwa pale ambapo wameshirikiana kuainisha dira yao wao wenyewe ya jinsi wanavyotaka jamii yao ikue, iendelee, na istawi kadili muda unavyokwenda. Dira ya jamii (pamoja na mpango wa matumzi ya ardhi) inaweza kuwasaidia wanajamii kubaini jinsi ambavyo wanataka ardhi na rasilimali zao zitumike, na kisha kufanya maamuzi yanayosaidia ufanikishaji wa dira hiyo.

Jamii inapokuwa na dira yake yenyewe kuhusu namna ambavyo itatumia ardhi na rasilimali zake kustawi na kukua, itakuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kufikia maafikiano pale mwekezaji atakapokuja akiahidi “maendeleo” kwa masharti ya mwekezaji.

Zoezi lifuatalo rahisi, linalotumia masaa matatu kuainisha dira, linaweza kuisaidia jamii ikubaliane kuhusu “dira ya siku za usoni,” na kisha kupanga hatua gani inaweza kuzichukua ili kufanikisha dira hiyo.



Wanajamii wanaweza kuamua jinsi jamii inavyoweza kustawi na kuendelea muda unavyokwenda, kulingana na vipaumbele na malengo yao wenyewe.



## ZOEZI LA KUAINISHA DIRA YA JAMII

**Nani anapaswa kuhusika:** Usianze mchakato wa kuainisha dira ukiwa na viongozi wachache tu au wawakilishi kutoka katika jamii: kuwe na angalau wanajamii 100–200—au asilimia kubwa ya kaya katika jamii—zishiriki kikamilifu. Wazee, vijana, wanawake, wanaume, wawakilishi kutoka katika vikundi vyenye watu wachache, na wadau wengine wote wa jamii wanapaswa kuhusishwa kikamilifu katika zoezi la kuainisha dira. Jamii nzima ikichangia mawazo kuhusu dira, basi jamii nzima itahisi hali ya “umiliki” na itajitoa kufanikisha dira hiyo.

**Jinsi ya kusikiliza sauti zote:** Pamoja na kwamba ni vyema zaidi kufanya zoezi hili katika kikundi kimoja kikubwa, katika baadhi ya mazingira, wanawake hawatazungumza kwa uhuru mbele ya wanaume. Katika hali kama hizo inaweza kuwa na tija zaidi kuigawa jamii katika vikundi viwili vya wanaume na wanawake (vijana wakiwekwa pamoja na wazee). Kwa maana hiyo, panga muda wa kukutana tena katika kikundi kimoja kikubwa, kutoa mrejesho, na kuweka pamoja dira zilizobuniwa na wanaume na wanawake katika vikundi vyao ili kupata dira moja pana ya jamii.



### Kueleza simulizi halisi

Jamii nyingi zina simulizi kuhusu namna ambavyo jamii iliundwa. Kujadili historia ya jamii inaweza kuwasaidia watu kuelewa umuhimu wa kulinda ardhi, rasilimali, mila, lugha na utambulisho wake. Kama muda ukiruhusu, waalike wazee wa jamii wasimulie jinsi jamii ilivyoanzishwa. Zoezi hili linasaidia kuikita jamii katika historia yake na inatoa sehemu nzuri ya kuanzia kwa ajili ya mchakato wa kuandaa dira. Simulizi ya halisi inaweza pia kuthibitisha uhalali wa jamii juu ya ardhi na rasilimali zinazotafutwa na mwekezaji.

**Hatua 1: Kukumbuka siku za nyuma.** Waombe wanajamii waeleze jinsi ardhi, rasilimali na mahusiano katika jamii yalivyokuwa siku za nyuma (miaka 30 hadi 50 iliyopita) wakati wazee wa leo walipokuwa watoto. Waombe wanajamii washirikishane kumbukumbu zao ndani ya kikundi. Andika kila kitu kinachosemwa. Hakikisha kwamba kila mmoja anapata nafasi ya kuzungumza—wazee wanakuwa na shauku sana ya kuongea katika majadiliano kama haya, wakati vijana wanaweza kuzungumza kuhusu mambo waliosimuliwa na mababu na mabibi zao kuhusu siku za nyuma. Baadhi ya maswali ya kuchochea mjadala ni pamoja na:

- ➔ Ardhi ya jamii ilikuwa inatumika vipi miaka kadhaa iliyopita?
- ➔ Ni rasilimali na vifaa gani ambavyo wanawake, wanaume, wasichana, na wavulana walikusanya kutoka katika ardhi ya pamoja?
- ➔ Rasilimali hizi zilikuwa nyingi kiasi gani? Ilichukuwa muda gani kupata na kukusanya rasilimali kama kuni na vifaa vya jadi vya kuezekea?
- ➔ Je, watu waliishi vipi na kufanya kazi pamoja ndani ya jamii? Wanaume na wanawake walihusiana vipi? Majirani walihusiana vipi?
- ➔ Kulikuwa na shughuli gani au sherehe za kimila zilizofanyika?
- ➔ Jamii ilifanyaje maamuzi kuhusu ardhi na rasilimali? Maamuzi na sheria hizi zilitekelezwa vipi? Je, viongozi wanasimamia vizuri ardhi ya jamii?
- ➔ Vijana walijifunzaje kuhusu mambo ya kimila?
- ➔ Wanajamii walijali nini zaidi? Vipambebe vyao vilikuwa ni nini?

### Hatua 2: Tafakari kuhusu wakati uliopo.

Waulize wanajamii wafikirie jinsi ambavyo ardhi, rasilimali, na mahusiano ya jamii yalivyo hivi *leo*. Baadhi ya maswali ya kuchochea mjadala ni pamoja na:

- ➔ Ardhi yenu ya jamii inatumikaje hivi sasa na inasimamiwa vipi?

- ➔ Je, kumekuwa na mabadiliko katika upatikanaji au wingi wa rasilimali ambazo wanawake, wanaume, wasichana na wavulana wanapata kutoka katika ardhi ya pamoja? Inachukua muda gani kutafuta na kukusanya rasilimali kama kuni na vifaa vya asili vya kuelekea?
- ➔ Je, watu wanaishije na kufanyakazi namna gani ndani ya jamii? Wanaume na wanawake wanahusiana vipi? Majirani wanahusiana vipi?
- ➔ Jamii yenu inafanyaje maamuzi kuhusu ardhi na rasilimali? Maamuzi na sheria vinatekelezwa vipi? Je, viongozi wanasimamia ardhi ya jamii vizuri?
- ➔ Mnajifunza vipi kuhusu mambo ya kimila na tamaduni zenu?
- ➔ Je, mmeridhika na hali iliyopo? Nini kinakwenda vizuri? Nini hakiendi vizuri?

**Hatua 3: Kufikiria kuhusu siku za mbele.** Kisha, waulize wanajamii ardhi na maliasili zao/mahusiano ya kijamii vitakuwaje miaka kama 50 ijayo, kwa wajukuu zao, kama mambo yataendelea kama yalivyo sasa hivi. Waombe wanajamii wafunge macho ili waweze “kuona” kwa uhalisia maono hayo katika akili zao. Wape watu muda wa kufikiria kuhusu hili —Usiharakishe hatua hii. Waombe watu washirikishane kile walichokiona wa jinsi siku za baadae zinavyoweza kuwa. Andika kile watu wanachosema. Baadhi ya maswali yanayoweza kuchochea majadiliano ni pamoja na haya yafuatayo:

- ➔ Je, ardhi na rasilimali zenu zitapatikana kwa urahisi kiasi gani na zitakuwa nyingi kiasi gani?
- ➔ Mazingira yenu yatakuwa mazuri kiasi gani (mito, udongo, misitu, milima, n.k.)?
- ➔ Watu watapata wapi chakula, vifaa vya kujengea, maji, dawa, na mafuta?



#### Ruhusu ukimya kwa muda ili mabadiliko yanatokee

Wakati mwingine, katika hatua hii, jamii inaweza kuwa katika hali ya ukimya mzito. Waache wakae kimya kwa muda kidogo ili hisia waliyo nayo ijengeke vizuri akilini. Huu ni muda muafaka kwa baadhi ya jamii na unapaswa kusimamiwa vizuri kwa moyo wa dhiti.

- ➔ Watu watahusiana vipi na kuishi pamoja?
- ➔ Watu watajikimu vipi?
- ➔ Je, watu watakuwa wanafuata mila na desturi?
- ➔ Mnajisikiaje kuhusu wajukuu zenu kuishi katika hali kama hii?

Mawazo ya washiriki yanapohama kutoka kumbukumbu za maisha ya nyuma kwenda kwenye maisha yanavyoweza kuwa baadae, hisia zao zinaweza kubadilika kutoka hisia za furaha zenye hamu ya mambo waliyozoea na kuwa hisia za huzuni na woga. Endapo watu wataonesha kukosa raha, sisitiza kwamba pamoja na kwamba hali ya sasa inaweza kuonekana kuwa mbaya, bado zipo njia za kubadilisha mambo ili kuhakikisha maisha ya baadae yenye maendeleo na usitawi kwa watoto na wajukuu wao. Wasiwasi kuhusu maisha ya baadae ambayo yana mashaka unaweza kubadilishwa kuwa nia ya kulinda ardhi, rasilimali, desturi na mila za jamii.

#### Hatua 4: Kuona maisha ya baadae yanayotarajiwa.

Waombe wanajamii wafunge macho kwa mara ya pili, na wafikirie vile ambavyo wangependa jamii yao iwe kwa ajili ya wajukuu zao katika miaka 30 au 50 ijayo. Kwa mara nyingine, wape dakika chache za kufikiria, kisha waombe washirikishane maono yao. Andika kila wanachokisema kwenye karatasi kubwa. Baadhi ya maswali ya kuchochea majadiliano ni pamoja na haya yafuatayo:

- ➔ Jamii inafananaje? Mandhari yakoje? Ubora wa maji, udongo na hewa vikoje? Ni rasilimali gani zinapatikana?
- ➔ Watu wanaishije na kufanya kazi pamoja ndani ya jamii? Wanaume na wanawake wanahusiana vipi? Majirani wanahusiana vipi?
- ➔ Jamii inafanyaje maamuzi kuhusu ardhi na rasilimali? Maamuzi na sheria vinatekelezwa?
- ➔ Kuna aina gani za miundombinu au huduma za umma ndani ya jamii?
- ➔ Ni aina gani za masoko, sherehe za kimila, na matukio yanayofanyika ndani ya jamii yenu? Vijana wanajifunza vipi kuhusu mambo ya kimila?
- ➔ Ni aina gani za shughuli za kujikimu ambazo watu watakuwa nazo?
- ➔ Hali ya ustawi wa jamii ikoje?



Ili kuzisaidia jamii ziweze kujenga maono ambayo yanajumuisha **uwekezaji unaoweza kufanyika na wanajamii au watu kutoka nje**, maswali mahsusi kuhusu uwekezaji yanaweza kuwa pamoja na haya yafuatayo:

- Je, kuna biashara zozote zinazoendeshwa katika jamii yenu? Nani anamiliki biashara hizo? Biashara hizo ni za kitu gani?
- Biashara hizo zinatoa aina gani ya ajira? Ni akina nani wanaajirwa? Wanajifunza stadi zipi?
- Je, biashara hizi zinalipa kodi, pango, au sehemu ya faida kwa jamii?
- Je, hizo biashara zimeboreshaje maisha katika jamii yenu? Ni zimefanya maboresho gani katika miundombinu ya jamii?
- Je, biashara hizi zimeathiri vipi mazingira—ubora wa maji, hewa, na udongo— na wingi wa rasilimali kama miti, wanyama pori, samaki na vifaa vya kujengea?

**Hatua 5. Kuandaa mpango kwa ajili ya wanajamii kufanikisha dira yao.** Kamilisha zoezi na “hatua zinazofuata” ambazo ziko wazi. Wanajamii wanapaswa kutafakari shughuli watakazofanya kufikia dira yao, kama vile kutenga eneo la msitu wa hifadhi kwa ajili ya matumizi ya wajukuu wao, kulinda chemchem za maji na mito, au kupanda miti. Kuandaa mpango kazi utakaowasadiia wanajamii kufikia dira yao:

- **Kukubaliana kuhusu vipaumbele vya siku za mbele.** Jamii zinatofautiana; wadau tofauti wanaweza kuwa na mawazo tofauti kuhusu nini kifanyike kwa ajili ya siku zijazo katika jamii. Mchakato wa kuandaa mipango unaweza kuisaidia jamii kushughulikia tofauti zao na kufikia maridhiano ambayo yanahakikisha kwamba maslahi ya vikundi yanazingatiwa katika juhudi za maendeleo ya jamii.
- **Kuamua nini cha kufanya ili kuelekea kwenye dira ya siku za mbele.** Mpango kazi wa jamii ulioandaliwa vizuri, unatoa hatua zilizo wazi, zinazotekelezeka, na ambazo zinaweza kupelekea ufanikishaji wa dira ya jamii. Mpango huo unawasaidia pia wanajamii kuamua njia bora ya kutenga rasilimali kama vile ardhi, muda, fedha, na ujuzi ili kufanikisha dira na kufikia malengo yake.

- **Kusaidia usimamizi mzuri wa ardhi na rasilimali za jamii na kulinda maslahi ya vizazi vijavyo.** Mipango kazi ya jamii, kama ilivyo kwa mipango ya matumizi ya ardhi, inaweza kuzisaidia jamii zifanye maamuzi yenye busara kuhusu namna ya kutumia ardhi na rasilimali zake kwa usawa na kwa njia endelevu.
- **Kufanya mashauriano yenye nguvu zaidi na wawekezaji watarajiwa.** Mpango kazi wa jamii—unaoambatana na ramani, mipango ya matumizi ya ardhi na sheria thabiti za jamii kuhusu namna ya kufanya maamuzi kuhusu uwekezaji—unaweza kuweka wazi kwa wawekezaji na maafisa wa serikali kwamba jamii ina vipaumbele vyake na dira ya siku za mbele na kwamba, uwekezaji wa nje ni lazima usaidie kufanikisha malengo na mpango wa jamii.

Baadhi ya maswali ya kuchochea majadiliano ni pamoja na haya yafuatayo:

- Ni nini vipaumbele vitatu vya juu vinavyohusu hatua ambazo jamii inaweza kuchukua katika mwaka huu?
- Ni aina gani za miradi ya ndani ambayo wanajamii wanaweza kuifanya sasa hivi ili kuanza kufanikisha malengo yenu? Ni miradi gani inapaswa kuwa sehemu ya mpango wa muda mrefu?
- Ni hatua gani ambazo wanawake wanaweza kuzichukua? Ni hatua gani ambazo wanaume wanaweza kuzichukua? Ni hatua gani ambazo wazee wanaweza kuzichukua? Ni hatua gani ambazo vijana wanaweza kuzichukua?
- Ni washirika gani au wataalamu gani kutoka nje ya jamii ambao mnaweza kuwaomba msaada? Je, kuna maafisa wa serikali ambao wanaweza kuwa na fedha ambazo mnaweza kuziomba na kuzipata kwa ajili ya maendeleo ya eneo lenu?

Mkutano unapoisha, piga picha maelezo yote uliyoandika kwa ajili ya kuweka kumbukumbu. Jamii inaweza kubandika dira iliyokubaliwa katika mkutano wa mashauriano ya ndani mahali ambapo kila mwanajamii anaweza kuiona, ili dira hiyo itumike kama njia ya kuwakumbusha kuhusu malengo ya kulinda ardhi na maliasili za jamii.

## KUELEWA THAMANI YA ARDHI NA RASILIMALI ZA JAMII KWA WANAJAMII

Ardhi ya watu wote kama vile maeneo ya malisho, misitu, na maeneo chepechepe—pamoja na rasilimali zilizopo ndani ya maeneo hayo—ina thamani kubwa kwa jamii. Hata hivyo, kwa wanajamii waliozoea kukusanya mahitaji muhimu kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kama kuni, dawa za mitishamba, na matunda pori na mboga kutoka katika maeneo haya, inaweza ikawa vigumu kuelewa ni kiasi gani maeneo haya yana thamani kwa kila kaya ndani ya jamii. Jamii isipothamini ardhi na rasilimali zake, kuna uwezekano mkubwa kwa wanajamii kukodisha ardhi yao kwa wawekezaji kwa thamani ndogo kuliko ile ambayo wanaipata kutoka katika ardhi hiyo. Kwa hali hiyo, wanajamii wanaweza kuwa maskini zaidi baadae kuliko kutajirika. Jamii zinazofahamu thamani ya ardhi zinaweza kuwa na nguvu zaidi ya kufanya mashauriano na wawekezaji na kujiandaa zaidi kufikia maridhiano yenye tija ili kupata mkataba wa haki na unaolinda maslahi yao.

Watetezi na viongozi wanaweza kuzisaidia jamii kufanya zoezi la mara moja, la masaa matatu hivi kupiga mahesabu ya gharama ya kurejesha rasilimali zinazowindwa au kukusanywa kwa wakati ule kutoka katika ardhi ya jamii. Zoezi hili linatoa makadirio ya kiasi cha fedha ambacho kingehitajika kwa kila familia kununua rasilimali kutoka sokoni ambazo ni muhimu kwa ustawi wa kaya, ikiwa jamii itakodisha misitu yake, maeneo ya malisho, au maeneo ya chepechepe kwa mwekezaji na wasiweze tena kutumia maeneo hayo bila malipo.<sup>1</sup>

Zoezi hili la tathmini ni vyema likafanyika katika mkutano mkuu wa jamii, unaohudhuriwa na wanaume, wanawake, vijana, na watu wanaojishughulisha na shughuli tofauti za kujikimu, wakiwemo wawindaji, wavuvi, na wengine ambao wanazifahamu vyema rasilimali za jamii. Mtetezi au kiongozi wa jamii anaweza kuwaongoza wanajamii kufuata hatua zifuatazo:

1. Kwanza, wanajamii watafakari na “kupaaza sauti” kuhusu orodha ya rasilimali zote ambazo jamii inazitumia au kuzikusanya kutoka katika misitu ya jumla, maeneo ya malisho, maeneo ya chepechepe, na mikondo ya maji. Baada ya kupata orodha kamili, *chagua rasilimali kati ya 8–10 zinazotumika zaidi kwa ajili ya kufanya mahesabu ya thamani.*
2. Baada ya hapo jamii itakadiria ni kiasi gani cha kila rasilimali kinatumika na familia moja “ya kawaida” kila wiki (tumia kipimo ambacho rasilimali hiyo inauzwa sokoni, kama vile mzigo/kifurushi/fungu, kapu, kisha ikadirie ni vipimo vingapi vya rasilimali hizo kila familia inatumia kwa wiki au kwa mwezi).
3. Kisha, kadiria gharama ya kila kipimo cha kila rasilimali kwa bei ya sokoni.
4. Halafu, kadiria familia ingepaswa kutumia fedha kiasi gani sokoni kununua kiasi cha rasilimali hizo kwa kila wiki, mwezi, na mwaka. (Kama rasilimali inatumika mara moja kwa mwaka, au mara moja kwa mwaka, ruka kipengele cha wiki na ujaze tu gharama ya mwezi au mwaka.)
5. Kisha, kadiria idadi ya familia zilizopo ndani ya jamii, uzidishe kiasi ambacho kila familia “ya kawaida” ingetumia mara *jumla ya idadi ya familia zote ndani ya jamii.*
6. Mwisho, kadiria gharama ya jumla ambayo jamii ingehitaji kutumia kununua mahitaji hayo ya lazima sokoni, kwa kutumia fedha za nchi na kwa dola za Kimarekani (fedha za kigeni ambazo wawekezaji wengi wanatumia).













Kielelezo kilichopo kwenye ukurasa mkabala na huu kinaonesha jinsi ya kuendesha zoezi hili. Mstari wa kwanza umejazwa kama mfano. Kielelezo hiki kinapaswa kichorwe kwenye karatasi kubwa ili wanajamii wote waweze kuona na kufuatilia makadirio na mahesabu yanavyofanyika. Wanajamii wanaweza kutumia vikokoteo vya simu zao za mkononi ili kumsaidia mtetezi anaeendesha zoezi kupata majibu sahihi ya mahesabu.

<sup>1</sup> Ni muhimu kuzingatia kwamba thamani hii ni tofauti na: 1) thamani ya ardhi na rasilimali kwenye soko la ardhi la kitaifa 2) thamani ya ardhi na rasilimali kwa wakazi watarajiwa au wanunuzi. Wanajamii wanatakiwa kutafuta msaada kutoka kwa wanasheria na wataalamu ambao wanaweza kufanya pia utafiti kuhusu thamani nyingine za kiuchumi.



(Washiriki ndio wanaamua rasilimali zipi ziorodheshwe kwenye mraba wa kushoto, lakini wawezeshaji wanapaswa kutoa mifano kama hii au ya rasilimali nyingine zinazotumika kama hazitatajwa na washiriki.)

Zilizotafutwa kutoka kwenye ardhi ya pamoja na maeneo ya maji na familia moja "ya kawaida"	Kipim (mzigo, kilo, n.k.)	Kipimo kinachotumiwa kwa wiki	Gharama kwa kila kipimo	Gharama kwa wiki	Gharama kwa mwezi (x4)	Gharama kwa mwaka (x12)
 Kuni	Mzigo mmoja	7	\$1	\$7	\$28	\$336
 Maji						
 Nyama pori						
 Samaki						
 Mboga #1						
 Mboga #2*						
 Dawa za mitishamba						
 Tunda mwitu #1*						
 Tunda mwitu #2						
 Nyasi za kuelekea						
<b>Jumla ya gharama ya chakula na rasilimali kwa familia moja "ya kawaida":</b>						
* Ongeza mistari ya ziada kwa ajili ya aina tofauti za mboga na matunda pori, asali, vifaa vya kujengea, n.k. – lakini hakikisha kwamba jamii inajumlisha vifaa vinavyotafutwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.						
<b>Jumla ya gharama ya chakula na rasilimali kwa familia moja "ya kawaida"</b> (jumla ichukuliwe kutoka hapo juu)	<b>Idadi ya jumla ya familia zilizopo ndani ya jamii</b>		<b>Gharama ya jumla ya rasilimali kwa jamii nzima kwa mwaka</b> (fedha za mahali husika)			
<b>X</b>			<b>=</b>			

Baada ya kumaliza mahesabu, ni muhimu kwa wanajamii kujaribu kufikiria jinsi ambavyo maisha yao yangekuwa endapo wangekuwa hawawezi tena kutumia ardhi yao. Watetezi wanaweza kuuliza maswali yafuatayo:

→ Je, mngekuwa hamna tena ardhi yenu, mngepata wapi kuni, vifaa vya kujengea, matunda pori na mboga, na rasilimali nyingine ambazo familia zenu zinazitegemea?

→ Mngekuwa hamna tena ardhi yenu, mngepataje fedha ya kununulia rasilimali sokoni?

→ Kwakuwa sasa mnafahamu thamani ya kile mnachokipata kutoka katika ardhi yenu ya jamii, mngekuwa tayari kukodisha ardhi hii? Kama jibu ni Ndiyo, bei gani ingekuwa halali, ukizingatia thamani ambayo tayari mnaipata kutoka katika ardhi hii?

## KUHAKIKISHA WA WANAJAMII WANAELEWA HAKI ZAO ZA ARDHI NA RASILIMALI

Kwa kawaida sheria ni ngumu kueleweka na zinaandikwa kwa namna ambayo ni vigumu kwa watu ambao sio wanasheria kuelewa. Watetezi wanaozisaidia jamii wanashauriwa kuandaa muhtasari rahisi wa ukurasa mmoja wa sheria za kitaifa na za kimataifa ambazo zinahusu ardhi ya jamii na haki za rasilimali katika muktadha wa mashauriano kati ya jamii na mwekezaji.<sup>2</sup> Muhtasari huu mfupi ni vyema ukaandikwa kwa lugha rahisi inayoeleweka kwa wanajamii husika. Nakala za muhtasari zilizojaladiwa kwa karatasi ya nailoni zinaweza kugawiwa kwa wanajamii ili waisome, washirikishane, na kufanya marejeo. Watetezi na wanajamii wanaweza pia kuandaa na kufanya maigizo mafupi na nyimbo ambazo zinatoa muhtasari wa sheria za kitaifa na za kimataifa ili kuwasaidia wanajamii kuelewa dhana muhimu, namna, na wakati gani wazitumie.

Sheria za nchi ambazo zinahusu haki ya ardhi na rasilimali za jamii huwa zinajumuisha mambo yafuatayo:

- **Katiba ya nchi**, ambayo inaeleza haki za mali za wananchi, ikiwemo haki ya kufidiwa kwa usawa pale ambapo Taifa linachukua ardhi kwa ajili ya mahitaji halali ya umma.
- **Sheria za nchi za mazingira, sheria za misitu, sheria za maji, na sheria za mipango ya matumizi ya ardhi.** Sheria hizi (pamoja na kanuni zake) kwa kawaida zinakuwa na ulinzi kwa ajili ya haki za ardhi na rasilimali za jamii.
- **Sheria za taifa za uwekezaji na kanuni zake ambazo zinaainisha taratibu za kutoa idhini ya serikali kwa ajili ya uwekezaji.** Jamii zinapaswa kufuatilia na kuhakikisha kwamba mwekezaji anayo haki kisheria kufanya shughuli nchini mwao. Kuelewa aina ya vibali na leseni ambazo

mwekezaji anapaswa kuomba kutoka serikalini kunaweza kuzisaidia jamii kufuatilia ili kuhakikisha kama serikali yao imetoa idhini zote zinazostahili kwa mwekezaji. Jamii zinatakiwa zihakikishe kwamba zinaelewa michakato ya serikali ya kuidhinisha miradi ya uwekezaji, zikiwemo sheria kuhusu usikilizaji wa kesi hadharani (public hearings) na mashauriano ya jamii. Jamii zinazoelewa hatua mbalimbali ambazo mchakato wa serikali ya uidhinishaji wa uwekezaji zinaweza kujaribu kuingilia ili kushawishi masharti ya uwekezaji, au kuishinikiza serikali kukataa mradi ambao utaminye maslahi yao.

- **Sheria za nchi au kanuni ambazo zinahitaji tathmini za kimazingira, kijamii, na/au haki za binadamu “tathmini za athari.”** Nchi nyingi zinazo sheria zinazowataka wawekezaji watarajiwa kufanya Tathmini ya Athari za Kimazingira (EIA), Tathmini ya Athari za Haki za Binadamu (HRIA), na/au Tathmini ya Athari za Kijamii (SIA).<sup>3</sup> Kwa kawaida, tathmini za athari zinakuwa na mapendekezo kuhusu jinsi ya kuepuka/kuzuia au kupunguza athari hasi zinazoweza kutokana na mradi kwenye eneo husika (ikiwemo hewa, maji, na ubora wa udongo), kwa afya ya jamii, na ustawi wa jamii, na kwenye haki za binadamu za wanajamii. Kwa kawaida, sheria za nchi zinaruhusu jamii ziombe kwamba matokeo ya tathmini hizi yawekwe hadharani; jamii zinaweza kutumia matokeo hayo wakati wa mashauriano na wawekezaji au kuiomba serikali au mahakama kulinda haki zake kama tathmini zinaonesha uwezekano wa kuwepo kwa athari hasi.

<sup>2</sup> Jamii pamoja na watetezi wao wanaweza kumwomba mwanasheria katika jamii aandike muhtasari wa sheria za nchi na za kimataifa bila malipo (pro bono). Aidha, wanafunzi wa sheria wanaweza kuwa na shauku ya kuandika muhtasari huo.

<sup>3</sup> Wakati mwingine Tathmini ya Athari za Kimazingira na Tathmini ya Athari za Kijamii zinafanyika kwa pamoja na zinaitwa Tathmini za Athari za Kimazingira na Kijamii au Tathmini za Athari za Kijamii na Kimazingira.





Jifunze na uulize maswali kuhusu haki za kisheria za jamii yako.

Haki nyingi zilizoelezwa katika sheria za nchi zinabebwa na kutekelezwa na **sheria za kimataifa, mikataba ya kimatafa na itifaki** ambazo serikali ya nchi zimetia saini au zimeridhia. Jamii zinaweza kutumia sheria hizi za kimataifa kutetea haki zake endapo serikali zao zinawapa vitisho.

### AZIMIO LA UMOJA WA MATAIFA LA HAKI ZA WAZAWA

**KIFUNGU 10** kinasema: “Wazawa hawataondolewa kwa nguvu kutoka katika ardhi au maeneo yao. Hakuna uhamishaji utakaofanyika bila kupata ridhaa huru iliyotolewa kabla ya tukio, kutokana na uelewa wa jambo husika na wazawa baada ya kukubaliana kuhusu fidia stahiki pale inapowezekana, ikiwa na uwezekano wa kurudi.” (Tazama pia Vifungu 11, 28, 29, na 32.)

Iliyo muhimu zaidi ni haki ya jamii ya kutoa **“Ridhaa Huru, Kabla, na iliyotokana na Uelewa wa jambo husika” (RHKU)**. Kwa wazawa na watu wa makabila, hii ni haki inayolindwa na sheria ya kimataifa.<sup>4</sup> Kwa kuongezea, miradi inayofadhiliwa na mikopo kutoka katika taasisi za kimataifa zinazotoa mikopo kama vile Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Asia, na Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) inahitaji Ridhaa Huru, Kabla, na iliyotokana na Uelewa wa jambo husika kabla mradi/uwekezaji haujaanza. Ridhaa Huru, Kabla, na iliyotokana na Uelewa wa jambo husika ni lazima pia itolewe kwa baadhi ya miradi ya uwekezaji. Kwa mfano, baadhi ya mashirika ya uthibitisho (kama mkutano wa kujadili Mafuta ya Mawese Endelevu ambapo kila mshiriki alichukuliwa kuwa na umuhimu sawa na mwingine) yanahitaji Ridhaa Huru, Kabla, na iliyotokana na Uelewa wa jambo husika ya jamii zote zinazotumia ardhi na rasilimali zao kwa pamoja zenye uwekezaji wa mafuta ya mawese. Baadhi ya makampuni pia yanahitaji Ridhaa Huru, Kabla, na iliyotokana na Uelewa wa jambo husika. Jamii zinapaswa kutafuta msaada wa kisheria ili kufahamu kama sera za kampuni zinahitaji kampuni ipate Ridhaa Huru, Kabla, na iliyotokana na Uelewa wa jambo husika kutoka kwa jamii kabla uwekezaji haujaanza.

<sup>4</sup> Haki ya Ridhaa Huru, iliyotolewa Kabla kutokana na Uelewa wa jambo husika inalindwa katika maazimio na matamko mengi, yakiwemo *Azimio Na 169 la Shirika la Kazi Duniani na Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Wazawa, na kupitia tafsiri ya Agano la Kimataifa juu ya Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR)* na baadhi ya mikataba ya kikanda.

Jamii zinapaswa kuelewa kwa makini maana halisi ya Ridhaa Huru, Kabla, na iliyotokana na Uelewa wa jambo husika: ni zaidi ya haki ya “kushirikishwa” kabla maafisa wa serikali hawajaidhinisha uwekezaji. Kwa usahihi zaidi:

- **“Huru”** inamaanisha kwamba ridhaa imetolewa bila kulazimishwa, kutishiwa, au kudanganywa kwa hila.
- **“Kabla”** inamaanisha kwamba jamii zinayo haki ya kuchukua muda kabla ya kuamua: jamii inapaswa ipewe muda wa kutosha kujadili uwekezaji unaopendekezwa kabla ya kufanya uamuzi. Wawekezaji na serikali ni lazima waheshimu michakato ya kutoa maamuzi ya jamii na wasiishinikize jamii kuharakisha uamuzi—hasa siku hiyohiyo ya pendekezo la uwekezaji. **Jamii zinaweza kudai zipewe muda wa kutosha kujifunza na kuelewa uwekezaji unaopendekezwa kabla hazijatoa maamuzi.**

- **“Uliotokana na uelewa”** inamaanisha kwamba jamii inayo haki ya kuelewa kuhusu mpango wa mwekezaji, ikiwa ni pamoja na aina, ukubwa, lengo, na eneo la mradi unaopendekezwa, pamoja na athari na hatari zozote za kiuchumi, kijamii, kimila, au kimazingira za mradi huo.
- **“Ridhaa”** inamaanisha haki ya kusema “hapana.”

#### AGANO LA KIMATAIFA JUU YA HAKI ZA KIRAIA NA KISIASA

- **KIFUNGU 19** kinasema: “Kila mtu atakuwa na haki ya kujieleza; haki hii itahusisha haki ya kutafuta, kupokea, na kusambaza taarifa za kila aina”
- **KIFUNGU 25(A)** kinasema: “Kila mwananchi atakuwa na haki na fursa ya kushiriki katika masuala ya umma.



Chini ya sheria za kimataifa, wanajamii wanayo haki kisheria kuwa na taarifa zote zinazohusu uwekezaji uliopangwa.



Chini ya sheria za kimataifa, watu binafsi na jamii pia zina **haki kisheria ya kupata taarifa na kushiriki** (tazama upate maelezo zaidi kuhusu haki ya kupata taarifa katika sehemu ya 9). Haki ya kujieleza imetafasiriwa kwa kumaanisha kuwa watu wanayo haki ya kutafuta taarifa zenye manufaa kwa umma, na serikali zao ni lazima zitoe taarifa hizo pale zinapombwa. Taarifa hizi zinaweza kujumuisha mikataba ya uwekezaji na athari za mradi kwenye mazingira na afya ya umma. Watu binafsi na jamii zina **haki ya kushiriki** pia katika masuala ya umma; hii inaweza kuelezwa kuwa watu wanayo haki ya kushawishi michakato katika maamuzi kuhusu uwekezaji unaoweza kusababisha athari kwao.

Nyaraka nyingine za kimataifa zinatetea pia mashauriano na jamii kabla uwekezaji haujaanza. Kwa mfano, *Miongozo Hiari isiyokuwa na kifungo kuhusu Usimamizi wenye wajibu wa Umiliki* inapendekeza kwamba wawekezaji na serikali zishauriane na “wamiliki wote wenye haki halali ya umiliki” kabla ya kufanya maamuzi au mapatano ambayo yataathiri usalama wa umiliki wao.

### MIONGOZO HII KWA AJILI YA USIMAMIZI WENYE DHAMANA WA UMILIKI INATAFSIRI “MASHAURIANO NA USHIRIKI” KAMA:

“Kujishughulisha pamoja na kutafuta msaada wa wale ambao, kuwa na haki halali za umiliki, kunaweza kuathiriwa na maamuzi, kabla ya uamuzi kufanyika, na kujibu michango yao; kuzingatia ukosefu wa uwiano katika nguvu za kufanya maamuzi kati ya pande tofauti na kuhakikisha ushiriki hai, huru, wenye ufanisi, wenye tija na ambao unatokana na uelewa wa jambo husika, wa watu binafsi na vikundi katika michakato ya maamuzi.”

Sheria za kimataifa zilionukuliwa hapa ni mifano michache tu ya sheria za kimataifa zinazolinda haki za jamii. Wanajamii pamoja na watetezi wao wanaweza kutafuta ushauri kutoka kwa mwanasheria au msaidizi wa kisheria kuhusu mapatano mengine ya kimataifa ambayo ya nalinda haki zao katika muktadha wa uwekezaji.



#### PATA USHAURI WA KISHERIA

1. hini ya sheria ya nchi, jamii yetu ina haki zipi juu ya ardhi na rasilimali zetu?
2. Je, serikali yetu inatambulika kwa kuheshimu haki hizo?
3. Ukizingatia sheria ya nchi, sisi kama jamii tuna nguvu kiasi gani za kisheria kumwomba mwekezaji afanye mashauriano na sisi na kuomba ridhaa yetu kabla hajatumia ardhi au rasilimali zetu?
4. Chini ya sheria ya nchi, sisi kama jamii tunayo haki ya kusema “hapana” kwa mwekezaji mtarajiwa? Je, tunayo haki madhubuti kutoa Ridhaa Huru, Kabla, na iliyotokana na Uelewa wa jambo husika?
5. Chini ya sheria ya nchi, sisi kama jamii tunayo haki ya kudai kodi au faida nyingine kwa matumizi ya ardhi na rasilimali zetu?
6. Je, sheria za nchi ama mikataba kati ya serikali na mwekezaji zinaeleza au kuweka kikomo kwenye kile tunachoweza kudai?
7. Ni michakato gani ya kisheria ambayo jamii inaweza kuitumia kuhakikisha utekelezaji wa mkataba, kama ikibidi? (Kama michakato hiyo haiwezi kutumika, haiwezi kutegemewa, siyo ya haki, faida ya kuwa na mkataba mzuri inaweza kuvurugwa na ukweli kwamba huenda jamii isiweze kulazimisha utekelezaji wa mkataba endapo kampuni haitaufuata.)

## 6.

## KUBAINISHA VIPAUMBELE VYA JAMII, KUSAIDIA MAAMUZI YA JAMII, NA KUTUNGA SHERIA NDOGO NDOGO

Maamuzi kuhusu kugawa au kutogawa ardhi na rasilimali za jamii na wawekezaji hayapaswi kuharakishwa. **Jamii isisubiri mpaka mwekezaji afike akitafuta ardhi na rasilimali ndipo ianze kufikiria kuhusu mambo gani yana manufaa kwa jamii au kutunga sheria na kupanga kuhusu namna ya kushauriana na mwekezaji ambae atafika.**

Wanajamii wanaposhauriana na wawekezaji watarajiwa baada ya kufikiria kwa makini, kama kikundi, kuhusu njia bora ya kuhakikisha maisha ya baadae ya jamii iliyoshamiri na kuendelea, kuna uwezekano mkubwa zaidi kwamba matokeo ya mashauriano kati ya jamii na mwekezaji yatapelekea utimilifu wa dira ya jamii inayotarajiwa.



Mpango wa matumizi ya ardhi unaoeleweka unaweza kuisaidia jamii ikue kwa namna endelevu.



## KUANDAA NA KUPITISHA SHERIA NDOGO NDOGO: KUANDIKA VIPAUMBELE VYA JAMII VILIVYOKUBALIKA NA MPANGO WA UFANYAJI MAAMUZI

Baada ya kujadili na kufanya mdahalo kuhusu maswali yaliyomo katika sehemu hii, **wanajamii wanatakiwa waandike yale waliokubaliana kama “sheria” au “sheria ndogo ndogo” ambazo zitafanya maamuzi na taratibu walizokubaliana yawe wazi kwa wanajamii wote, viongozi, maafisa wa serikali, na wawekezaji.** *Japokuwa ni vyema zaidi kwa jamii kuwa na mikutano mingi ya kujadili na kufanya midahalo kuhusu sheria zake na namna ya kushauriana na wawekezaji watarajiwa, mchakato unaweza kufupishwa na kuwa na siku chake tu za majadiliano.* Mchakato wa haraka wa kuandika sheria unaweza kuwa na hatua zifuatazo:

- **Mkutano 1:** Jamii, ikiwa kundi moja kubwa, inabunga bongo kwa pamoja au kutaja kwa sauti sheria zote zilizopo na zile zilizokuwa zinafuatwa siku za nyuma ambazo zinahusu *usimamizi wa ardhi na rasilimali na utoaji wa maamuzi wa jamii.* Kila sheria iliyopo inayotajwa kwa sauti inaandikwa kwenye karatasi kubwa. **Hii ni rasimu ya kwanza ya sheria ndogo ndogo.** (Kuhakikisha ushiriki wa wote, jamii inaweza pia kujigawa katika vikundi vidogo vya wanaume, wanawake, vijana, ambavyo vitaandaa orodha zao, na kisha orodha zote zinaweza kuunganishwa.)
- **Mkutano 2:** Jamii inapitia rasimu ya kwanza ya sheria ndogo ndogo, inaongeza sheria mpya, inafuta sheria za zamani ambazo hazina faida tena, na kubadilisha sheria zilizopo ambazo ni lazima ziboreshwe ili ziendane na sheria za nchi. Sheria zipitiwe kwa mada, mada moja kwa wakati. Mada zinaweza kuwa pamoja na sheria kuhusu maji, mito, chemichemi, na maziwa; sheria kuhusu misitu; sheria kuhusu maeneo ya malisho; sheria kuhusu njia, barabara, na haki ya njia; sheria zinazoeleza ni maamuzi gani ambayo viongozi wanaweza kufanya na yapi ambayo hawawezi kufanya pekee yao, na maamuzi gani ambayo yanapaswa kufanywa na jamii nzima kama kundi; sheria kuhusu nini kifanyike endapo mwekezaji atakuja kutafuta ardhi (imeelezwa zaidi hapa chini); sheria kuhusu haki za wanawake, haki za wanaume, haki za watoto, na haki za watu kutoka katika makundi yenye watu wachache, n.k.

**Majadiliano yaendeleo mpaka jamii ikubaliane kwamba wana rasimu ya 2 iliyokamilika.** Kutegemeana na muda jamii ilio nao, inaweza kuchukua mkutano mmoja au mikutano mingi iliyosambaa katika wiki kadhaa kukamilisha rasimu ya 2. Mchakato huu ni vyema ufanyike taratibu, ili kuwapa wanajamii muda wa kufikiri na kutafakari kuhusu kile ambacho ni muhimu kwa maslahi yao ya muda mrefu. Hata hivyo, kama mwekezaji anafika siku za karibuni, majadiliano na maamuzi haya yatapaswa kukamilika haraka sana.

- Baada ya rasimu ya 2 ya sheria ndogo ndogo kukamilika, isambazwe kote katika jamii, ili kuhakikisha kwamba watu wote wanakubali, hata wale ambao hawakuweza kuhudhuria mikutano ya kujadili sheria (au “sheria ndogo ndogo”). Mtezezi, msaidizi wa kisheria, au mwanasheria wanapaswa wapitie sheria hizo kuhakikisha kwamba hazipingani na sheria ya nchi. Baada ya kufanya marekebisho yanayotakiwa ili kuingiza maoni ya wanajamii na mawazo ya kuhakikisha kwamba sheria haziendi kinyume na katiba ya nchi, jamii sasa itakuwa na rasimu ya mwisho, iliyokubalika na kila mmoja. **Hii itakuwa ni rasimu ya 3 ya sheria ndogo ndogo.**
  - **Mkutano 3:** Wanajamii wanazipitisha sheria, au sheria ndogo ndogo hizo, kwa kura rasmi ya maridhiano (makubaliano ya asilimia 100%) au kura ya juu (makubaliano ya asilimia 66%). Matokeo ya kura yanapaswa kuandikwa kwenye kumbukumbu yakiambatanishwa na picha, video, na sahihi za wanajamii. Maafisa wa serikali za mitaa wanaweza kualikwa kushuhudia upitishaji wa sheria hizi na kutia saini au kugonga muhuri rasmi sheria hizo kuzipa “uzito wa kiofisi.”
- Wawekezaji watarajiwa na maafisa wa serikali wanapokuja kutafuta ardhi, jamii inaweza kuwapatia nakala ya sheria ndogo ndogo na kuwataka viongozi wa jamii, wawekezaji na maafisa wa serikali wa mkoa wafuate sheria za jamii zilizokubalika pamoja na mchakato unaopendelewa na jamii wa mashauriano na utoaji wa idhini.**

Hususani kwa uwekezaji wa baadae, sheria au sheria ndogo ndogo za jamii, zinaweza kuwa na mada zifuatazo:

## JE, UWEKEZAJI WA NJE UNAKUBALIKA? KAMA JIBU NI NDIYO, WAPI, NA KWA KUTUMIA VIGEZO NA MASHARTI GANI?

Jamii zinapaswa kuanza kufikiri iwapo wataruhusu mwekezaji atumie ardhi ya jamii, na kwa masharti gani. Jamii inapaswa kuitisha mikutano ya kujadili na kuamua kuhusu mambo yafuatayo:

- **Je, wanajamii wako tayari kiasi gani kumruhusu mwekezaji atumie ardhi ya jamii?** Baadhi ya jamii zinaweza kuamua kwamba kamwe hazitaruhusu ardhi yake itumike na mwekezaji, wakati jamii nyingine zinaweza kukaribisha uwekezaji wa nje. Wanajamii wanaweza kugawanyika. Kwa mfano, wazee wanaweza wasipende kukodisha ardhi kwa wawekezaji, lakini vijana wakawa radhi kubadilishana ardhi na rasilimali za jamii kwa ajira na fursa nyinginezo. Wanajamii wanapaswa kusaidiwa kutoa sauti zao zote hadharani katika mdahalo wa umma wa wazi, kisha wakazingatia matakwa ya wadau katika kutafuta ufumbuzi ambao unawakilisha mawazo na matakwa ya vikundi vyote.
- **Je, ni kampuni za aina gani au shughuli zipi ambazo zitakubalika?** Wawekezaji na makampuni yanatofautiana. Jamii inaweza kuamua kwamba itaikatalia kampuni ya kukata magogo kuwekeza, na kuikubalia kampuni ndogo inayozalisha vifaa kama vile mafuta ya nazi au matunda yaliyokaushwa ambazo zitanunua mazao ya kilimo kutoka kwa wakulima. Wanajamii wanapaswa kufahamu kwamba shughuli za biashara ambazo zitaaidia jamii kustawi zinaweza kukubalika na zile ambazo zinaweza kuiumiza jamii hazitaruhusiwa.
- **Ardhi ipi inaweza kutumika na mwekezaji, na ipi inapaswa kubaki chini ya udhibiti wa jamii?** Kama jamii iko radhi kuruhusu kampuni ifanye shughuli katika ardhi yake, ni maeneo gani mahususi ambayo yanaweza kutumika kwa ajili ya matumizi ya kampuni? Ni ardhi ipi haiwezi kutumika na kampuni? Jamii zinapaswa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi inayobainisha maeneo mahususi ambayo yanaweza kufaa kwa ajili ya aina fulani za shughuli za kibiashara.
- **Ni kwa muda gani jamii iko tayari kugawana ardhi yake na mwekezaji?** Kama jamii ikikubali

kumruhusu mwekezaji atumie sehemu ya ardhi na rasilimali zake, mwekezaji aruhusiwe kuvitumia kwa muda gani? (miaka 5? miaka 10? miaka 25?) Pamoja na kwamba mwekezaji atapenda kuwa na mkataba wa muda mrefu, jamii zinaweza kuomba mikataba ya muda mfupi zaidi. Mikataba ya muda mfupi ina maanisha kwamba, kama uwekezaji unaiumiza jamii, basi jamii hiyo haitasubiri kwa muda mrefu mno mpaka mradi huo ufike mwisho (au mpaka iweze kufanya mashauriano ya kupata mkataba mzuri zaidi, endapo mwekezaji ataomba mkataba uendeleo). Sheria za nchi zinaweza kuweka ukomo wa mikataba ya aina hii.

- **Ni sheria zipi ambazo wawekezaji wanaofanya shughuli katika jamii wanapaswa kuzifuata?** Ikiwa jamii inakubali kumruhusu mwekezaji atumie sehemu ya ardhi na rasilimali zake, inatakiwa kuweka sheria zilizo wazi kuhusu jinsi ambavyo mwekezaji anapaswa kufanya shughuli zake, ikiwemo kutoachia kemikali ziingie kwenye mfumo wa maji wa mahali husika, kutotupa taka zilizotokana na uzalishaji na matakataka ndani ya eneo la jamii, kutumia vichuja hewa ili kuzuia uchafuzi wa hewa, kukutana kila baada ya robo mwaka na jamii kujadiliana kuhusu changamoto au matatizo na kutafuta ufumbuzi, n.k.

## NAMNA GANI JAMII ITAFANYA MAAMUZI YA KUMRUHUSU AU KUTOMRUHUSU MWEKEZAJI KUTUMIA ARDHI YA JAMII?

Kabla mwekezaji yeyote hajajitokeza, watetezi na wanajamii wanapaswa kuainisha kwa pamoja au kuweka michakato ya kufikia maamuzi iliyo wazi na iliyonyooka (isiyo na mizengwe). Majadiliano ya kufikia maamuzi kuhusu hilo yanapaswa kujibu maswali yafuatayo:

- **Ni nani atafanya maamuzi?** Je, ni wakazi wote, wakiwemo wanawake, vijana, na watu kutoka katika vikundi vyenye watu wachache watapewa fursa ya kutoa maoni yao na kusikilizwa? Nini kitatokea iwapo kikundi chenye watu wachache kikipishana au kikiwa na maoni tofauti na walio wengi?
- **Tofauti katika maoni zitashughulikiwa vipi?** Jamii itazungumzia suala hilo wenyewe kwa wenyewe mpaka maridhiano yapatikane, au itatafuta watetezi, viongozi wa dini, viongozi wa kimila, au maafisa wa serikali za mitaa kujibu maswali muhimu na kufanya upatanisho? Ni mikakati gani mingine, iwe ya kimila au ya kisasa, inaweza kutumika? (Tazama sehemu ya 7 hapa chini).

- **Uamuzi utafanyikaje?** Ni lazima asilimia ngapi ya wanajamii wakubali? Je, uamuzi utafanyika kwa kura ya muafaka (makubaliano ya asilimia 100%), kura ya juu (asilimia 66%), au kura ya jumla (51%)?
- **Uwajibikaji wa viongozi?** Je, jamii inaweza kutumia mchakato gani endapo viongozi wao au baadhi ya wazee/viongozi wakiamua kukodisha sehemu kubwa ya ardhi bila ushirikishaji na uidhinishaji wa jamii?



**Inashauriwa kwa msisitizo kwamba jamii itunge sheria yenye maneno kama yafuatayo: “ni lazima angalau asilimia [taja kiasi]% ya wanajamii washiriki katika maamuzi ya kukodisha ardhi ya jamii kwa wawekezaji. Mikataba yoyote na wawekezaji ambayo imetiwa saini na wazee au viongozi pekee yao bila ushiriki kamili na ridhaa ya angalau asilimia [taja kiasi]% ya wanajamii utachukuliwa kama mkataba batili na jamii.”**

## **MKAKATI UPI UTATUMIKA KUSIMAMIA TOFAUTI NA MIGOGORO YA KIJAMII?**

Kuna uwezekano kwamba fursa mpya na ahadi zinazotoka kwa wawekezaji na/au serikali zikachukuliwa kwa namna tofauti na watu tofauti ndani ya jamii. Kwa mfano, wanajamii ambao hawana ardhi au walio na ardhi isiyo na rutuba ya kutosha wanaweza kuwa na shauku zaidi kuliko wanajamii wenye uwezo zaidi kuhusu fursa za ajira ambazo uwekezaji wa nje unaweza kuleta. Hii inaweza kusababisha migogoro ndani ya jamii, ambayo itadhoofisha nafasi ya jamii wakati wa kushughulika na wawekezaji wa nje na maafisa wa serikali. Kwa tahadhari ya uwezekano wa kutoka mgogoro ndani ya jamii kuhusu namna ya kusimamia mradi tarajiwa wa uwekezaji, jamii inapaswa kuandaa haijatokea—Mpango wa kushughulikia migogoro ili kuweza kusimamia mitafaruku.

Kama jamii tayari inao mfumo wenye ufanisi wa kutatua migogoro ya ndani, mfumo huu uelezwe vizuri na kuandikwa ili taratibu za kufuata zijulikane na kila mmoja. Hatua nyingine zozote za ziada ambazo zinaweza kusaidia kusimamia migogoro, kuhusiana na uwekezaji wa nje ipitishwe na kuongezwa. Pamoja na kwamba mipango ya kutatua migogoro inaweza kutofautiana kati ya jamii moja na nyingine, mpango huo angalau uweze kujibu maswali yafuatayo:

- **Ni mtu gani ambae hafungamani na upande wowote, anaheshimika, na ambae anaweza kusaidia watu walio katika mgogoro kufikia makubaliano kwa amani kuhusu jinsi ya kushughulikia ombi la mwekezaji?** Huyu anaweza kuwa kiongozi wa dini, mtu wa makamo, afisa wa serikali anaeaminika, msuluhishi mbobezi, msaidizi wa kisheria, au mwakilishi kutoka katika shirika la kijamii.
- **Je, migogoro kati ya wanajamii kuhusu uamuzi wa kushauriana na mwekezaji mtarajiwa au la na namna ya kuafikiana nae itasuluhishwaje?** Kuna mchakato gani uliopo wa kushughulikia migogoro ndani ya jamii— migogoro ndani ya jamii inashughulikiwaje hivi sasa? Je, mchakato huu unatosheleza, au unahitaji kubadilishwa ili uweze kushughulikia migogoro kuhusu uwekezaji wa nje? Mikakati gani ya ziada au mazungumzo gani ya kutatua migogoro inaweza kuhitajika?

**Ni lazima jamii iwe na uhakika kwamba inao mfumo ulioandaliwa vizuri wa kutatua migogoro ya ndani miongoni mwa wanajamii au vikundi vya wadau na kupata suluhu kwa tatizo husika.** Pamoja na kwamba siyo kila mmoja anaweza kukubali, inawezekana kusikia maoni yote na kufikia muafaka ili kuhakikisha kwamba maslahi ya wadau wote yanalindwa. Ni vyema kuunda mchakato wa kutatua migogoro ambao unaruhusu kila upande wa mgogoro kueleza msimamo wao, mahitaji yao, matakwa yao na imani zao kwa namna ambayo kila mtu anaweza kuelewa. Huenda ikawa lazima kuzungumza kwa ukweli na uwazi kuhusu sababu za ndani za kihistoria, kitabaka, kikabila au kimaisha za mgogoro huo. Baadhi ya mikakati ya kutafuta suluhu ni pamoja na:

- **Kuitisha mikutano ya jamii ili kuendesha mazungumzo ya wazi.** Hii inahusisha kuwaleta pamoja watu wote wanaohusika na mgogoro na kwa ajili ya majadiliano ya pamoja. Lengo ni kusikia maelezo yote na kubaini chanzo cha tatizo, madhara yaliyotokea, na sheria zote husika. Sheria za kimila pamoja na sheria rasmi zinaweza kujadiliwa. Mwezeshaji anaweza kuendesha majadiliano hayo ili kuhakikisha kwamba kila mmoja anapata fursa ya kuzungumza na kwamba maelezo yote muhimu yanatolewa.
- **Kuomba msaada kutoka kwa viongozi na maafisa wa serikali wanaoaminika.** Viongozi wanaoheshimika wanaweza kutumia nguvu walio nayo kusaidia pande zote kutatua migogoro kuhusu ardhi.



⇒ **Upatanishi.** Upatanishi ni mchakato unaoongozwa na mpatanishi ambao hafungamani na upande wowote. Wapatanishi wanaweza kuwa wanasheria, wasaidi wa kisheria, viongozi, au wanajamii waliopata mafunzo ambao wanaheshimika. Kazi ya mpatanishi ni kuwakumbusha wajumbe wa pande zote kuhusu sheria husika, kurahisisha mawasiliano katika pande husika, kutafuta eneo la makubaliano, na kusaidia katika kubaini suluhisho. Upatanishi huwa unatumika pale ambapo majadiliano yamekwama na watu wahusika wa mgogoro wanahitaji msaada kutoka kwa mtu ambao hajinasibishi na mgogoro. Upatanishi unaweza ukahitajika katika mazingira yafuatayo: pale watu wanapokuwa na hisia kali au kusababisha ugumu wa kufikia muafaka; pale ambapo mawasiliano hayaendi vizuri; pale ambapo kuna hali ya kutokukubaliana kuhusu mambo na taarifa muhimu; na pale ambapo kuna ukosefu mkubwa wa uwiano katika nguvu ya kufikia maamuzi kati ya wahusika. Lengo la mpatanishi linapaswa kuwa kusaidia kupata suluhu ambayo itanufaisha pande zote zinazohusika katika mgogoro.

## JAMII ITAOMBA NINI KAMA MBADALA KWA KURUHUSU MATUMIZI YA ARDHI NA RASILIMALI ZAKE?

Sheria za nchi nyingi zinaruhusu jamii ziombe wawekezaji wawafanyie/wawape kitu fulani kwa kutumia ardhi na rasilimali zake. Lakini sio kila wakati jamii inakuwa inafahamu mambo yote ambayo wanaweza kuomba kama “mafao” kama fidia/malipo kwa matumizi ya ardhi yake. Kwa mfano, jamii zinaweza kuomba mafao yanayotolewa mara moja kama ujenzi wa shule ama kituo cha afya, lakini zikashindwa kuomba vitu kama waalimu, madaktari, vitabu, umeme, na dawa ambavyo vinahitajika kuhakikisha kwamba hizo shule na zahanati zinaendeshwa kwa ufanisi. Wakati huo, gharama za mafao yanayotolewa mara moja ni sehemu tu ya thamani ya ardhi inayotolewa kwa mwekezaji.

Wanajamii wanaweza kusaidiwa kufikiria kuhusu kudai kodi ya kutumia ardhi au asilimia ya faida inayopatikana ambayo thamani yake inakaribiana zaidi thamani ya ardhi yao, ili kuhakikisha kwamba jamii itastawi kutokana na uwekezaji, huku ikitiliwa maanani kwamba mafao ambayo jamii inadai ni lazima yaendane na hali halisi ya masharti ya uwekezaji.

## BAADHI YA MANUFAA YANAYOWEZA KUDAIWA KUTOKA KWA WAWEKEZAJI<sup>5</sup>

1. **Kodi** au ada ya kutumia ardhi na rasilimali za jamii.
2. **Mirahaba au kiwango kisichobadilika cha sehemu ya faida za mwaka** zinazolipwa kwa jamii.
3. **Miundombinu kama vile vituo vya afya** (ikiwa ni pamoja na dawa, madaktari na wauguzi), shule (ikiwa ni pamoja na vitabu, waalimu na makaratasi), jengo la mikutano, barabara, na visima vya maji.
4. **Umeme** (umeme unaoendeshwa na upepo, mionzi ya jua) na miundombinu ya **mawasiliano** (kuunganishwa na huduma ya simu na intaneti).
5. **Ajira na mafunzo** ya kazi kwa idadi maalumu ya wanajamii, wakiwemo wanawake, vijana, watu wanaoishi na ulemavu, na watu kutoka kwa vikundi vyenye watu wachache.
6. **6.Mikataba na wanajamii ya utoaji wa vifaa na huduma, kwa mfano,** kununua chakula kutoka kwa wakulima katika jamii kwa ajili ya wafanyakazi wa kampuni.
7. Manufaa yoyote mengine ambayo jamii inaona yanaweza kuisadia kutimiza malengo yao ya siku za usoni.



Mkakati wa kutatua migogoro utaisaidia jamii kutatua migogoro au kushughulikia hali ya kutoelewana kati yao huku wakijadiliana kilicho bora kwa maendeleo ya jamii.

5 Ili kupata maelezo kamili ya mafao ambayo jamii inaweza kuomba, na kwa masharti gani, tazama Mwongozo 2, sehemu ya 8.

Haitoshi kwa jamii kufikiria tu kuhusu mafao itakayoomba—swali kuhusu **namna gani na lini mafao hayo yatatolewa ni muhimu** pia. Kutegemeana na aina ya mafao jamii imepanga kuomba, wanajamii wanapaswa pia kufikiria maswali yafuatayo:

→ **Ulipaji wa kodi/ada na ugawanaji wa faida.**

- Endapo jamii inataka ilipwe na mwekezaji kwa kutumia ardhi na rasilimali zake, italipwa kwa ujumla na kutumia fedha hizo kwa ajili ya miradi ya jamii, au kila familia itapewa sehemu ndogo ya jumla ya fedha zitakazolipwa?
- Kama fedha zitalipwa kwa familia moja moja, jamii itahakikishaje kwamba fedha hizo hazilipwi tu kwa wakuu wa kaya wanaume, lakini inagawanywa kwa namna ambayo wanafamilia wote wanafaidika?
- Endapo jamii italipwa kama jamii, nani ataamua fedha hizo zitumike vipi? Fedha hizo zitasimamiwaje?
- Fedha hizo zitahifadhiwa wapi na nani atakuwa na mamlaka ya kuzitoa?
- Jamii itapataje taarifa kuhusu matumizi ya fedha hizo?
- Ni taratibu gani zinaweza kuwekwa kuhakikisha kwamba viongozi hawaingizi suala la rushwa katika matumizi na usimamizi wa fedha hizo?

→ **Maendeleo ya miundombinu na huduma za jamii.** Kama jamii inataka mwekezaji ajenge shule, hospitali, barabara, au daraja, basi inabidi jamii ifikirie kabla kuhusu nini hasa inachotaka kuomba:

- Nani atajenga?
- Je, patakuwa na tarehe ya kikomo ambayo miundombinu hiyo inapaswa kuwa imekamilika?
- Je, ijengwe kwa kutumia vifaa maalum?
- Jengo au miundombinu hiyo ijengwe wapi?
- Adhabu kwa mwekezaji asipokamilisha mradi wa miundombinu itakuwa nini?
- Je, mwekezaji atalazimika kufanya au kulipia matengenezo ya mara kwa mara ya miundombinu hiyo?
- Nani atawalipa wafanyakazi wa hospitali, shule au taasisi nyingine?

Ni muhimu kukumbuka kwamba kwa kawaida, **utoaji wa miundombinu na huduma nyingine zinazohusiana ni jukumu la serikali.** Si nia ya kampuni kuingilia jukumu la serikali la kutoa miundombinu na huduma muhimu, kwasababu inaweza kuifanya serikali ikalegea zaidi katika kutimizia jukumu lake la kutoa huduma kwa jamii katika siku za usoni. Aidha, punde kampuni itakapoondoka kutoka katika eneo (au hata wakati bado ipo hapo), inaweza isiwe na uhakika hasa nani atagharamia na kutunza huduma ya miundombinu baada ya kujengwa.

→ **Ajira.** Mara nyingi wawekezaji huahidi kwamba watatoa ajira lakini wanaajiri wananchi wachache tu kutoka katika jamii au wanaajiri wananchi wenye kipato kidogo tu, wakati mameneja wanatoka sehemu zingine. Jamii zinazoomba mwekezaji atoe ajira zinapaswa kuwa tayari kuomba idadi maalumhususi ya ajira za kudumu na za muda, idadi maalum ya ajira zinazohitaji ujuzi (kama vile nafasi za menejimenti au ajira za ofisini), mishahara maalum kwa kila nafasi, na mafao ambayo yanaambatana na ajira, kama vile mafunzo kazini. Jamii zinapaswa kudai kwamba asilimia fulani ya wafanyakazi ipatikane kutoka ndani ya jamii; idadi kubwa ya wafanyakazi wa kiume kutoka nje inaweza kuleta tatizo la ulevi, kamari, ubakaji, na tabia nyingine hasi. Jamii inapaswa kufikiria kabla kuhusu mambo maalum yanayohusiana na maombi yao; kwa mfano:

- Asilimia ngapi ya wafanyakazi wote lazima watoke kutoka katika jamii?
- Asilimia ngapi ya nafasi za menejimenti lazima zijazwe na watu kutoka katika jamii?
- Wafanyakazi watalipwa mara ngapi?
- Je, wananchi katika jamii watapewa msaada wa kujengewa ujuzi na mafunzo kazini?
- Aina gani za mifumo ya kushughulikia migogoro kati ya wafanyakazi itakuwepo endapo wafanyakazi watatendewa vibaya au kutolipwa, au endapo kampuni itawatendea vibaya wananchi katika jamii?



# b

## MWEKEZAJI ANAPOFIKA KUTAFUTA ARDHI

- |  |    |   |    |
|--|----|---|----|
| 7. Kuelewa haki ya jamii ya kuhusishwa katika mashauriano  | 32 | 10. Kukamilisha mchakato wa mashauriano: kufanya uamuzi kuhusu kukataa uwekezaji au kupatana na mwekezaji | 41 |
| 8. Kuhakikisha kwamba jamii inahusishwa katika mashauriano kwa namna yenye tija                            | 35 | 11. Kujiandaa kuanza mashauriano kwa ajili ya mkataba kati wa jamii na mwekezaji                          | 45 |
| 9. Kupitia taarifa zote za kisheria, na kitaalamu na za kifedha kuhusu kampuni na uwekezaji unaopendekezwa | 38 | 12. Kuanza mashauriano  | 49 |





Uhusikaji wa jamii na mwekezaji kwa kawaida huanza pale kampuni – mara nyingi ikiambatana na maafisa wa serikali—inapotembelea jamii kuitaaruifu kuhusu mradi unaopendekezwa. **Jamii inapaswa kutafuta ushauri wa msaidizi wa kisheria au mwanasheria mara moja.**

Haipendezi, mwekezaji na/au serikali wakiitaaruifu jamii kuhusu mradi ambao tayari umekwishapitishwa na maafisa wa serikali kuu. Au, wawekezaji wanaweza kufika katika jamii wakiwa na baadhi ya viongozi, wakiwahonga au kuwashinikiza kutoa ridhaa kwa niaba ya jamii.

Inapendeza, mwekezaji na/au serikali wakianza mchakatao mrefu wa mashauriano na mazungumzo na jamii. Katika mazingira kama hayo, mchakato wa mashauriano kati ya jamii na mwekezaji utajumuisha mikutano na fursa kwa wananchi katika jamii kuomba na kupitia taarifa muhimu kuhusu mradi unaopendekezwa, kutoa madukuduku yao, na kushawishi maamuzi yanayohusu mradi unaotarajiwa. Sehemu iliyobaki ya mwongozo huu inatoa maelezo ya michakato hiyo.



## USITIE SAINI KITU CHOCHOTE AU KUTOA RIDHAA KWA PUPA

Jamii inapofuatwa na mwekezaji mtarajiwa na/au serikali wakitafuta ardhi, isiharakaishe kutoa ridhaa ya mdomo au kusaini kitu chochote. Pamoja na kwamba jamii inaweza kuwa na shauku ya kusema “ndiyo” kwa maafisa wa serikali, ambao baadhi yao wanaweza wakawa watu wenye nguvu au wanaoogopwa, jamii inapaswa kuahirisha uamuzi hadi mkutano mwingine, kisha ikatafuta msaada wa kisheria na kitaalamu mara moja.

## KUELEWA HAKI YA JAMII YA KUHUSHISHWA KATIKA MASHAURIANO

Kabla mradi haujabuniwa wa wakilishi wa kampuni na/au maafisa wa serikali wanatakiwa wakutane na wanajamii husika ili kuutamulisha rasmi mradi unaopendekezwa, kutoa taarifa, na kujifua kuhusu mahitaji ya jamii. **Mara nyingi mkutano huu huchukuliwa kama “mashauriano ya jamii”.** Kwa baadhi ya nchi mashauriano na jamii ni hitaji la kisheria. Aidha, kama ilivyobainishwa sehemu ya 5 hapo juu, sheria za kimataifa na/au sera za mashirika yanayotoa mikopo huenda zikahitaji “Rishaa huru, kabla, na iliyotokana na uwelewa wa jamii” itolewe; mashauriano na jamii ni sehemu kuu ya rishaa hii.

Mashauriano yaliyo bora (kamilifu) yanaitegemeza jamii nafasi ya kushawishi uingizaji wa vipengele muhimu katika muundo wa mradi unaopendekezwa. Kwa kawaida, mashauriano na jamii hayawezi

kufanyika wakati mwekezaji anakutana na jamii kwa mara ya kwanza; bali kama *mwendelezo wa vikao* ambavyo vitaipatia jamii taarifa muhimu zitakazowasaidia kuelewa kwa kina wigo na malengo ya uwekezaji.

Mashauriano lazima yajumuishe jamii yote kwa pamoja ili isikie maelezo kuhusiana na mradi unaopendekezwa, kisha yawape nafasi wanajamii kuuliza maswali, kupitia nyaraka na kuujadili uwekezaji miongoni mwao. Baada ya kukutana na wawekezaji na kupata nafasi ya kuwa na vikao vya ndani ambavyo vinaruhusu majadiliano ya faragha ya jamii, wanajamii wanweza kukubaliana na uwekezaji kama ulivyopendekezwa, kukataa uwekezaji, au kutoa mrejesho kuhusu uwekezaji unavyoweza kuboreshwa ili ukubalike na jamii.



Kamwe usitie sainsi katika hati zozote kwa pupa. Hakikisha haki ya jamii ya kutoa ridhaa huru, kabla, na iliyotokana na uwelewa wa jamii husika inazingatiwa.

**Kwa bahati mbaya mara nyingi mashauriano haya yanaendeshwa katika mazingira yasio na uwiano wa nguvu ya kufanya maamuzi:** wawekezaji wanafika kwa mara ya kwanza wakiwa wameambatana na maafisa wa serikali ambao huieleza jamii kwamba “wanahusishwa katika maamuzi” na kudai kwamba jamii iseme “ndiyo” hapo kwa papo. Kwa hakika, wawekezaji na maafisa wa serikali wengi wanaweza kuendesha “mashauriano” kama fursa za *kutoa taarifa tu* kwa jamii kwamba uwekezaji unafanyika. Jamii nazo zinaweza kujiona kwamba hazina namna bali kukubali mradi ambao tayari umekwihapitishwa na serikali. Mambo yanaweza kufanya “mashauriano” yoyote yawe batili ni haya yafuatayo:

**1. Jamii zinaweza zikalazimishwa kwa kutumia vitisho au ukatili, kugeuzwa wahalifu, au kukamatwa kwa makosa yasiojulikana na serikali au na mawakala wa mwekezaji.** Jeshi la taifa, polisi, au “majambazi” wa kukodishwa wanaweza kutumika kuwatisha watu, kuchoma nyumba na mali, na kutumia mbinu za kikatili ili kuwanyamazisha wananchi au upinzani. Mikakati kama hiyo inaweza kutumika kupata ridhaa ya jamii au kuwazuia wananchi wasidai taarifa au mafao mazuri zaidi. Vile vile, wawekezaji wanaweza kutumia rushwa, kwa kuwahonga viongozi wa jamii ili kusaini fomu za ridhaa, au kuzungusha “karatasi za mahudhurio” kwenye mikutano kisha wakadai kwamba zinawakilisha saini za wananchi waliotoa ridhaa. “Mashauriano” ya aina hii yanaweza kutumika na kampuni na/au serikali ili kutoa picha kwa vyombo vya nje vyombo vya kimataifa vya uthibitishaji wa viwango kwamba jamii zimetoa ridhaa kwa moyo.

**PATA  
USHAURI  
WA KISHERIA**

Je, sheria katika nchi yako inamtaka mwekezaji au serikali ishauriane na jamii? Ni nini hasa mwekezaji anapaswa kufanya wakati wa mashauriano? Kama hakuna sheria au viwango vya kurejea, bado jamii inaweza kuomba au kudai mashauriano yenye tija na kutaka taarifa kutoka kwa kampuni au serikali.

**2. Wawekezaji na maafisa wa serikali wanaweza wasiwape wanajamii taarifa za kutosha ili jamii ziweze kutathmini kwa undani faida na hasara za uwekezaji unaopendekezwa.** Jamii zinaweza kushinikizwa na serikali kukubali ahadi ambazo hawazielewi vizuri. Mwekezaji anaweza asiwaeleze wanajamii mambo muhimu kuhusu mradi wa uwekezaji, ambayo ni muhimu kwao ili waweze kuandikiana mkataba ambao utakuwa na manufaa ya kweli kwa jamii. Mifano ya taarifa muhimu ambazo zinaweza zisitolewe ni kama zifuatazo:

- Thamani ya ardhi sokoni na rasilimali ya jamii;
- Faida ya mwaka ambayo mwekezaji atapata kutokana na mradi;
- Thamani ya jumla ya mradi; na
- Athari zinazotarajiwa kwenye maji, hewa, misitu na afya ya jamii na wanajamii.

Hata pale taarifa zinapotolewa, zinaweza zisiwasilishwe katika lugha ambayo jamii inaielewa. Matokeo yake, wanajamii wanaweza wasiwe na taarifa kamili kuhusu mradi wa uwekezaji unaopendekezwa na athari zinazoweza kutokea kutokana na mradi huo kwenye mazingira, afya na katika ustawi wao.

**3. Wawekezaji na serikali wanaweza pia kuziomba jamii zitie saini kwenye mikataba ambayo haieleweki au ambayo haina maelezo ya kutosha ambayo haijumuishi maelezo yaliyo wazi kuhusu mipaka ya ardhi inayokodishwa;** ratiba na ahadi za dhati za malipo au mafao; marekebisho kwa ajili ya kuzingatia kupanda kwa gharama za maisha kwa siku za usoni malipo ya pango; au maelezo yaliyo wazi kuhusu namna ambavyo jamii inaweza kumwajibisha mwekezaji kufanya malipo ya mafao kwa wakati na kwa ukamilifu, kulinda mazingira, na masharti muhimu ya mkataba.

Hivyo basi **jamii inapaswa kutafuta msaada wa msaidizi wakisheria, mwanasheria, mtetezi anaeaminika kutoka katika shirika lisilo la kiserikali, au afisa wa serikali wakati wa mashauriano. Na jamii isitie saini mahali popote au kukubali jambo lolote mpaka mchakato wa mashauriano ukamilike.**



## KUTAFUTA MSAADA WA KISHERIA NA WA KITAALAM WAKATI WA MAZUNGUMZO NA Wawekezaji

Wanasheria, wataalam wa mazingira, wachumi, wataalamu wenye uzoefu na maendeleo ya jamii, haki za binadamu, uchambuzi wa masuala ya fedha na/au mashauriano na wawekezaji, na wataalam wengine wabobezi wanaweza kusaidia kushughulikia tofauti zilizopo katika wingi wa taarifa walizo nazo na nguvu ya kufanya maamuzi kati ya jamii na wawekezaji. Wanaweza pia kusaidia jamii ili zipate mikataba iliyo na usawa na haki zaidi kati ya jamii na mwekezaji. Wataalam hao wanaweza kufanya mambo yafuatayo:

- Kuzisaidia jamii zifahamu haki zao za kisheria chini ya sheria za taifa na za kimataifa;
- Kupata na kuelewa taarifa muhimu za kitaalamu, zikiwemo mipango ya biashara ya wawekezaji na matokeo ya Tathmini za Athari za Kimazingira, Kijamii, au Haki za Binadamu;
- Kubaini hatari na faida zinazoweza kutokana na mradi tarajiwa wa uwekezaji;
- Kupitia rasimu ya mkataba na kusaidia kuukamilisha;
- Kutoa ushauri kuhusu masuala tatanishi ya kisheria (yaani yasiyoelezeka kwa urahisi);
- Kuendesha mashauriano shirikishi yanayohusisha watu wote;
- Kuisiadia jamii wakati wanapokuwa na mazungumzo na mwekezaji; na
- Kuafikiana na wawekezaji kutokana uelewa wao na uwezo walio nao.

Hata hivyo, mawakili na wanasayansi huwa wanatoza ada kubwa sana kwa saa au kwa siku, na **malipo kwa ajili ya kufidia muda wa wataalamu hawa yanaweza kuwa changamoto** kwa jamii. Watetezi wa jamii wanaweza kuiunganisha jamii na mashirika ya kitaifa, au mashirika yasiyo ya kiserikali ya kimataifa au mitandao ya wataalam ili kutoa huduma hizi *bila malipo* kwa wateja na jamii zenye kipato kidogo. Ili **kupunguza gharama, wanajamii**

wanaweza kupatiwa mafunzo wawe wasaidizi wa wa kisheria ambao watafanya kazi kwa karibu na mwanasheria kutoa taarifa za kisheria kwa jamii, kusuluhisha migogoro, na kusaidia mahitaji ya kisheria ya jamii katika kipindi chote cha mashauriano kati ya jamii na mwekezaji.<sup>6</sup>

Aidha, serikali, mwekezaji au taasisi nyingine inaweza kutoa msaada wa kisheria au kulipia msaada huo. **Katika mazingira kama hayo, kuwa makini!** Endapo serikali au kampuni inalipa gharama za mwanasheria au mtaalamu kuisadia jamii, jamii inapaswa kufanya yafuatayo:

- **Kudai kwamba jamii yenyewe ndio ichague mwanasheria, hata kama mwekezaji analipa mshahara wake.** Kama kampuni inalipa gharama za mwanasheria wa jamii, ni lazima pawepo na utaratibu wa malipo ili kuhakikisha kwamba malipo ya mwanasheria hayategemeani na uthibitishaji wa kazi zake na kampuni. Fedha zinaweza kulipwa kabla ya huduma kutolewa kwenye akaunti ambayo siyo ya jamii wala ya mwekezaji au akaunti inayodhibitishwa na mwekezaji.
- **Kuwa makini kuhakikisha kwamba mwanasheria au mtaalamu hatoi ushauri ambao unalinda maslahi ya kampuni au ya serikali.** Wanajamii wanapaswa kufanya maamuzi na kuweka malengo ambayo mwanasheria au mtaalamu wao atawasaidia kuyafikia.
- **Kuweka masharti ya malipo ya mwekezaji au serikali kwa ajili ya msaada wa kisheria kwa jamii katika Mkataba wa Makubaliano (MOU)** ambao unaeleza wazi jinsi fedha hizo zitakavyolipwa, kwa nani, fedha zinaweza kutumika vipi, na haki za jamii (kwa mfano, haki ya kupata ushauri wa siri, kuchagua nani atoe msaada wa kisheria, kuamua kama inataka kuendelea kushauriana na mwekezaji au la) na majukumu. Mkataba huu wa makubaliano unapaswa kutamka wazi kwamba fedha kwa ajili ya msaada wa kisheria ambazo mwekezaji au serikali imelipa *siyo* malipo ya ridhaa ya jamii kuhusu uwekezaji.

<sup>6</sup> Ili kupata mwongozo wenye maelezo kamili kuhusu jinsi ya kuanda mpango wa wasaidizi wa wanasheria, tazama <https://namati.org/resources/developing-a-community-paralegal-program/>.

## KUHAKIKISHA JAMII INAHUSISHWA KIKAMILIFU KATIKA MASHAURIANO

Kabla ya kuanza mchakato wa mashauriano, watetezi wanapaswa kuwasaidia wanajamii kubaini kama wanayo haki kisheria chini ya sheria ya nchi kukataa mradi. Mambo yanayoipa nguvu au kudhoofisha haki ya jamii ya kukataa mradi uliopendekezwa ni haya yafuatayo:

- » **Kama jamii ni mmiliki halali wa ardhi na rasilimali chini ya sheria ya nchi**, na mradi unahusu uwekezaji katika kilimo, misitu au uzalishaji. Kama jamii inamiliki ardhi yake, inaweza kuwa na haki ya kukataa kuikodisha au kuingia katika mkataba na mwekezaji mtarajiwa.
- » **Kama ni mradi madini au unahusu rasilimali zilizopo chini ya ardhi ambazo ziko chini ya udhibiti wa serikali** pekee yake, basi **huenda jamii isiwe na haki ya kukataa mradi ule** na inaweza kutia mkazo katika kuafikiana ili ifikie makubaliano ambayo hayaiumizi sana jamii.



Viongozi wa jamii hawapaswi kukutana na wawekezaji watarajiwa pekee yao. Mikutano na wawekezaji inapaswa iwe wazi na wanajamii wote wawe huru kuhudhuria na kuuliza maswali.

Katika hali yoyote, watetezi na wanajamii wanaweza kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha kwamba mashauriano halali yanafanyika, kama vile:

1. **Kukataa kutoa ridhaa ya hapo kwa papo na kutafuta msaada wa kisheria.** Kama mwekezaji ataiomba jamii iridhie jambo ambalo jamii haielewi au haikubaliani nalo au inaipa jamii mkataba kwa ajili ya kutia saini, jamii inapaswa kumweleza mwekezaji kwamba:

- Bado hawajaridhia mradi wa mwekezaji;
- Wanayo haki ya kutafuta ushauri wa kisheria kabla ya kutia saini chochote au kutoa ridhaa; na
- Bado hawako tayari kufanya mashauriano na kwamba wanahitaji muda na taarifa zaidi kabla hawajatoa uamuzi wa jamii kuhusu ombi la kampuni.



2. **Kuweka kumbukumbu za kila mashauriano na wawekezaji kwa kutumia video au kwa maandishi.** Muhimu zaidi, jamii inapaswa kuandika, kuredodi video au sauti (kwa kutumia simu ya mkononi) kila mashauriano na mwekezaji na wawakilishi wake, hata mazungumzo ya kwenye simu. Jambo lolote mwekezaji analowaambia wanajamii, na kila kinachojadiliwa kati ya jamii na mwekezaji, ni lazima kiandikwe *na* kupigwa picha ili kuwa na kumbukumbu ya maandishi na ya kidigitali. Jamii inatakiwa iweke nakala za dondoo, barua, barua pepe, au ujumbe mfupi wa maandishi ambavyo jamii inatuma au kupokea kutoka kwa mwekezaji.<sup>7</sup> Kumbukumbu hizi zinaweza kutumika katika madai ya kisheria kama ushahidi wa maudhui ya mashauriano yote kati ya jamii na mwekezaji.

3. **Kubaini mahitaji ya kisheria kwa ajili ya mashauriano.** Watetezi wanaweza kubaini ni nini sheria ya taifa inahitaji kwa ajili ya mashauriano, kisha akawasaidia wanajamii kuikumbusha kampuni na serikali kuhusu masharti hayo ya kisheria na kuomba sheria itekelezwe ipasavyo. Kama hakuna sheria kama hiyo, watetezi wanaweza kutazama sera, sheria na masharti ya ndani ya kampuni, au vipimo vya nje ambavyo kampuni ni lazima ivizingatie, kama vile vipimo kutoka katika mifumo ya uthibitishaji au vipimo vinavyohitajika na mabenki ambayo yanatoa fedha kwa makampuni.

- Kwa mfano, kama kampuni inalima mitende na imethibitishwa na Mkutano wa Kujadili Mafuta ya Mawese Endelevu (RSPO), basi jamii inaweza kudai taarifa zaidi kuhusu uwekezaji unaopendekezwa na kwamba kampuni itasubiri Ridhaa Huru, Kabla, na iliyotokana na Uelewa itolewe, kwasababu *Kanuni na Vigezo vya Mkutano wa RSPO kwa ajili ya Uzalishaji wa Mafuta ya Mawese Endelevu* unahitaji kampuni zito taarifa (Kanuni 1) na kupata Ridhaa Huru, Kabla, na iliyotokana na Uelewa ya jamii (Kanuni 2.3).

Mifumo mingine ya uthibitishaji, na vipimo vya mambo yanayohusiana na fedha ina masharti yanayofanana. Watetezi wanaweza kutafuta msaada kutoka kwa shirika lisilo la kiserikali la kitaifa au kimataifa kuchunguza ni taasisi gani ya kifedha inayofadhili mradi na ni kanuni gani ambazo sheria za taasisi hizo zinahitaji.

7 Kuwa na kumbukumbu kutathibitisha kile kilichojadiliwa na kukubalika. Uwekaji wa dondoo na nyaraka, kama vitu vya kukumbushia ahadi zilizotolewa, unaweza kusaidia sana wakati wa mchakato wa mashauriano. Nyaraka kama hizo zinaweza pia kusaidia endapo patatokea migogoro au hali ya kutoelewana kati ya kampuni na jamii, au pale jamii ikiamua kuishitaki kampuni mahakamani.



4. **Kudai kwamba mchakato wa uhakika wa mashauriano ufuatwe.** Watetezi wanaweza kuisaidia jamii kudai kwamba mashauriano yafanyike kulingana na njia bora. Hii inamaanisha kwamba mashauriano:

- Yafanyike *kabla* serikali haijaidhinisha mradi uendele;e;
- Yafanyike mapema iwezekanavyo wakati wa hatua ya kubuni na kuainisha mradi;
- Yaruhusu jamii itoe **au ikatae** kutoa ridhaa ilio huru, kabla ya shughuli kuanza, na inayotokana na uwelewa wa hali husika;
- Yatoe fursa kwa jamii kujifunza kuhusu mradi na **kushawishi maamuzi** kuhusu mradi;
- Yafanyike katika lugha inayotumika katika jamii
- Yaendeshwe kulingana na sheria na mila za jamii husika;
- Yatoe fursa kwa wanajamii wote, wakiwemo wanawake, vijana, na watu kutoka katika makundi yaliyosahaulika kushiriki; na
- Yawe na ufadhili wa kutosha (ikiwezekana na wao wenyewe) ili kuiwezesha jamii itafute msaada wa kisheria na kitaalamu na kujenga uwezo wao wa kushughulikia ukosefu wa uwiano wa nguvu ya kufanya maamuzi kati ya jamii na kampuni.



5. **Kutoruhusu viongozi wa jamii kupitisha makubaliano bila kuishirikisha jamii.**

Mara nyingi wawekezaji na maafisa wa serikali wanaowasaidia hupendelea kukutana pekee yao na kiongozi wa jamii au kikundi cha viongozi au wazee wanaume. Ni rahisi zaidi kushawishi, kutisha, au kuhonga watu wachache kuliko kupata idhini halisi kutoka kwa jamii nzima. Jamii zinapaswa kutumia juhudi zote kuhakikisha kwamba viongozi wao hawafanyi mikutano ya pekee yao ya siri na wawekezaji. Watetezi wanaweza kuzisaidia jamii kuunda sheria zao ambazo zinahitaji ushiriki kamilifu wa jamii katika maamuzi yanayohusu uwekezaji na kudai kwamba viongozi waitishe mkutano mkuu wa jamii nzima kila mwekezaji anapofika kujadili uwekezaji unaopendekezwa.

Endapo viongozi watafanya maamuzi kuhusu uwekezaji bila kuishirikisha jamii, jamii inaweza kutafuta msaada wa mwanasheria kuchukua hatua dhidi ya viongozi hao. Katika mazingira mengine, jamii zimeweza kuwashawishi viongozi wao (kwa kufanya marejeo kwenye sheria ndogo ndogo za jamii na kwa kutumia mbinu za kuwaaibisha, n.k.) kukutana na wawekezaji na kufuta makubaliano au kudai ushiriki kamilifu wa jamii katika mashauriano.

Endapo kampuni itaonekana kutokubali kuishirikisha jamii katika mashauriano kwa namna yenye tija, basi jamii na watetezi wake wanaweza kuamua kuchukua hatua ambazo zitamulika hali iliyopo, kama vile kutumia vyombo vya habari kueleza kinachoendelea, kufanya utetezi wa moja kwa moja na wadau wa kampuni, kutafuta msaada kutoka kwa washirika wenye ushawishi wa kitaifa na wa kimataifa, kutafuta msaada kutoka kwa maafisa wa serikali wanaoaminika, na njia nyinginezo za hatua za moja kwa moja. Katika mazingira mengine, uamuzi wa kuchukua hatua za moja kwa moja utumike tu pale ambapo njia nyingine zimeshindikana, kwani imeshatokea jamii ikafanyiwa ukatili kwa kutangaza hali halisi.

## KUPITIA TAARIFA ZOTE ZA KISHERIA, KITAALAMU NA KIFEDHA KUHUSU KAMPUNI NA UWEKEZAJI UNAOPENDEKEZWA

Ili kufanya maamuzi yanayotokana na uelewa kuhusu jinsi ya kumjibu mwekezaji wakati wa mchakato wa mashauriano (na, endapo jamii itaamua kuingia katika mashauriano na mwekezaji, hii ifanyike wakati wa mchakato wa mashauriano pia), ni lazima jamii iweze kupata na kuelewa taarifa kuhusu mwekezaji, mradi unaopendekezwa, na athari zote chanya na hasi zinazoweza kutokea kutokana na mradi husika. Kuwa na taarifa hizi kutawaweka wanajamii katika nafasi nzuri zaidi kuamua kuingia katika mashauriano na mwekezaji au mambo wanayoweza kudai wakati wa mashauriano.

Wanajamii wanatakiwa kutafuta msaada kutoka kwa wanasheria na wataalamu ambao wanaweza kuwasaidia kuomba hizi taarifa, kufanya uchunguzi kuhusu uwekezaji na historia ya kampuni, waanzilishi wake, wakurugenzi, na wafadhili, na kuwaeleza yale yaliyoandikwa katika nyaraka (mara nyingi zinaandikwa kwa lugha ngumu kueleweka kwa makusudi) kwa lugha ambayo wanajamii wote wataweza kuielewa.



Kutana pamoja kama jamii kupitia taarifa zote kuhusu mwekezaji mtarajiwa na mradi wa uwekezaji kabla ya kukubali kugawa ardhi yoyote ya jamii.

1. Kwa kuanzia, jamii na watetezi wake wanatakiwa **kumwuliza mwekezaji maswali kadhaa moja kwa moja**. Maswali hayo yanaweza kuwa pamoja na:

- Kampuni inayotafuta ardhi inaitwaje?
- Je, kampuni hiyo inafanya shughuli zake nchini kihalali? (Kama jibu ni Ndiyo, omba kuona nyaraka zinazotoa idhini ya serikali.)
- Ni aina gani ya uwekezaji umepangwa kufanyika? Nishughuli gani zimepangwa kufanyika katika ardhi hiyo?
- Ni ardhi gani mwekezaji anataka kutumia kwa uwekezaji huo? Kwanini mwekezaji amechagua ardhi hii mahsus?
- Ni kipindi cha muda gani ambacho mwekezaji anaomba kukodi ardhi? Au mwekezaji anatafuta kununua ardhi?
- Mwekezaji anatarajia kupata faida gani?
- Ni athari gani za kimazingira na kijamii ambazo zinaweza kutokea kutokana na uwekezaji?
- Uwekezaji huu utaleta faida gani kwa jamii?
- Uwekezaji huo utaathiri vipi maendeleo na ustawi wa wanajamii?
- Mwekezaji amepanga kushirikiana na kuwasiliana vipi na jamii?

2. Jamii zinatakiwa pia zimwombe mwekezaji pamoja na serikali **wawape nakala za nyaraka zifuatazo**:

- **Tathmini ya kubaini kama mradi unatekelezeka:** Sheria za nchi zinahitaji wawekezaji wafanye “tathmini za utekelezekaji wa mradi” kuchunguza kama mradi unaopendekezwa unatekelezeka na unaweza kuleta faida au kufikia matokeo yaliyopangwa. Wanajamii wanaweza kuomba kupitia tathmini ya utekelezekaji wa mradi ili iwasaidie kuelewa kama mradi unaweza kushindwa au kufanikiwa; taarifa hii inaweza kuwasaidia wanajamii kuepuka kufanya mashauriano na kuingia mkataba na wawekezaji ambao miradi yao ina uwezekano mkubwa wa kushindwa.
- **Mpango wa Biashara wa mwekezaji:** Mara nyingi wawekezaji wanatakiwa kuwasilisha mpango wa biashara kwa serikali kabla mradi wao wa uwekezaji haujapitishwa. Mipango hii ya biashara inapaswa kutoa taarifa kuhusu namna mwekezaji alivyopanga kuendeleza

ardhi, ikiwemo mpango kazi wenye maelezo kamili na ratiba ya utekelezaji. Mpango wa biashara unapaswa kuwa na taarifa kuhusu faida kwa mwaka na/au faida baada ya kipindi fulani (angalau miaka kadhaa). Maelezo haya yanaweza kuisaidia jamii kuelewa namna ambavyo mradi unaweza kuwaathiri na kiasi gani cha fedha ambacho mwekezaji anatarajia kupata.

- **Vibali na leseni:** Mara nyingi wawekezaji wanatakiwa kupata vibali au leseni mbalimbali kutoka serikalini ili kuendesha shughuli kama vile kutafuta maji au kuvuna mbao. Vibali na leseni hizo zinamtaka mwekezaji afanye (au asifanye) mambo kadhaa kwenye eneo au karibu na eneo la jamii. Jamii zinashauriwa kutoamini kauli ya mwekezaji kwamba wana idhini ya serikali kutumia ardhi, maji, au misitu, na wanatakiwa kudai waoneshwe leseni na vibali husika. Mwekezaji akikataa, basi wanajamii wanaweza kupata taarifa hizi kutoka kwa wakala husika za serikali; wanaweza kutuma maombi ya “Uhuru wa kupata Taarifa” (yanayoelezwa hapa chini) ili wapate taarifa hizo.

- **Mkataba kati ya mwekezaji na serikali kuhusu mradi unaopendekezwa.** Katika baadhi ya mazingira, ni lazima kampuni iingie mkataba na serikali ili kutekeleza uwekezaji uliopangwa. Wanajamii na watetezi wao wanatakiwa kuomba nakala za mkataba wowote uliofanywa kati ya serikali na mwekezaji ili kuona ni haki zipi na majukumu gani ya kimkataba ambayo yamekwishakubaliwa kati ya serikali na mwekezaji. Maudhui ya mkataba kati ya mwekezaji na serikali yanaweza kupunguza au kuongeza nguvu ya jamii ya kujadiliana na mwekezaji kuhusu bei au malipo. Kwa mfano, katika nchi ambazo serikali ndiyo mmiliki wa ardhi ambayo itatumika na mwekezaji na mwekezaji amekwishatia saina mkataba na serikali, inawezekana jamii isiweze kushiriki katika michakato ya ufanyaji wa maamuzi kuhusu uwekezaji. Hata hivyo, jamii ambazo zitaathirika kutokana na uwekezaji zinapaswa kuhusishwa katika mashauriano na mashaka waliyo nayo kushughulikiwa.

Kuhusiana na msaada kwa jamii, ni muhimu kuelewa yaliyomo katika mkataba wa mwekezaji na serikali: jamii inaweza kugundua kwamba mkataba kati ya serikali na mwekezaji inamtaka mwekezaji atoe msaada



wa aina fulani kwa jamii. Taarifa hii inaweza kuisaidia jamii kumwajibisha mwekezaji atoe msaada huo, awape wanajamii fursa ya kueleza njia ambayo wangependa kupewa msaada huo, na ikiwezekana kuomba msaada wa ziada zaidi ya huo ambao mwekezaji amekwishatakiwa kuutoa kulingana na mkataba. Kwa upande mwingine, mkataba kati ya serikali na mwekezaji unaweza kujumuisha masharti ambayo yanapunguza ulinzi ambao jamii ingesitiza kupewa au msaada ambao ingeweza kuomba.

- **Ripoti za mchakato wa kubaini masuala ya kimazingira yanayopaswa kuingizwa katika tathmini ya mazingira na Tathmini za Athari (zikiwemo za kimazingira, kijamii, na Tathmini ya Athari za Haki za Binadamu):** Environmental scoping reports are often carried out in the early stages of project planning, before a full impact assessment is conducted. Taarifa hizi zinatoa tathmini fupi ya hatari za kimazingira ambazo mradi unaopendekezwa unaweza kusababisha na mapendekezo kadhaa kuhusu jinsi ya kuepuka/kuzuia au kupunguza athari hasi zinazoweza kutokea. Ni vyema kupitia ripoti hizi, kwani Tathmini za Athari zinaweza zisikamilike kabla mashauriano hayajaanza. Jamii zinaweza kuahirisha zoezi la kutia saina mkataba wowote mpaka waone matokeo ya Tathmini zote za Athari pamoja na mpango wa mwekezaji wa kukabiliana na hatari zilizobainishwa zinazoweza kutokea.
- **Sifa ya mwekezaji, mwenendo wake, au utendaji wake katika miradi mingine:** Jamii zinaweza kuomba taarifa kuhusu miradi mingine iliyotekelezwa na mwekezaji, zikiwemo nyaraka zinazoonisha utendaji wa miradi hiyo baada ya muda. Taarifa hii inaweza kusaidia kuonesha jinsi ambavyo kampuni inafanya kazi na kama imejitoa kuhakikisha kwamba shughuli zake zina manufaa kwa jamii, zinahakikisha haki za binadamu za jamii, na kuzingatia sheria za mazingira.
- **Taarifa kuhusu nani anaufadhili uwekezaji unaopendekezwa.** Mara nyingi, kampuni za uwekezaji ni sehemu ya makampuni “mama” yenye majina tofauti. Aidha, miradi mikubwa ya uwekezaji inatafuta ufadhili kutoka katika vyanzo vingi tofauti. Watetezi wanaweza

kuzisaidia jamii kugundua na kuona nani ameahidi kutoa fedha kwa ajili ya uwekezaji unaotarajiwa, na kampuni “mama” ya kampuni hiyo ni ipi. Taarifa hii inaweza kuisaidia jamii kutetea maslahi yake pale ambapo kampuni husika haina sifa nzuri.

Taarifa hii inatakiwa itolewe katika muundo unaorahisisha matumizi yake na iwe katika lugha ya jamii husika, na ikiwezekana iambatane na picha na video ambazo zitasaidia jamii ielewe taarifa hiyo.

**Endapo taarifa itazuiliwa, jamii na watetezi wake wanaweza kutuma maombi ya ‘Uhuru wa Kupata Taarifa’ na kudai taarifa kuhusu uwekezaji unaopendekezwa.** Iwapo serikali au kampuni itazuia taarifa kuhusu uwekezaji kutoka kwa jamii, watetezi wanaweza kuzisaidia jamii kutuma maombi ya “uhuru wa kupata taarifa” wakidai kwamba serikali itoe taarifa hiyo. Zaidi ya nchi mia moja zimepitisha sheria zinazohusu uhuru wa kupata taarifa, ambazo zinaipa umma haki ya kudai takwimu zinazoshikiliwa na serikali. Huenda ikawa lazima kutafuta msaada wa mwanasheria ambae amebobea katika maombi ya uhuru wa kupata taarifa asaidie kubaini ni taarifa zipi ambazo jamii ina haki ya kuzipata na jinsi ya kuzipata.

Omba **nakala ya nyaraka zote zinazohusika zitolewe kwa jamii ili wazisome kwa makini, wazielewe na wazichambue.** Kama hili haliwezekani, watetezi au wanajamii wanaweza kupiga picha kila ukurasa wa nyaraka hizo kwa kutumia simu ya mkononi na kisha wakazituma zichapishwe kwa ajili ya kupitiwa kwa uangalifu. Jamii inaweza ikahitaji msaada wa wanasheria, wasaidizi wa kisheria, na wataalam ili kuelewa yaliyomo kwenye nyaraka hizo. Wanajamii wanatakiwa waombe kwamba wapewe muda unaokubalika iliwapitie, maelezo yote ya uwekezaji unaopendekezwa.

Mwisho, kuongezea kwenye taarifa iliyomo kwenye nyaraka, **watetezi na viongozi wa jamii wanaweza kufanya utafiti kuona jinsi ambavyo miradi mingine inayofanana na mradi unaopendekezwa imetekelezwa** (na mwekezaji au makampuni mengine), na athari za miradi hiyo kwa jamii na kwa mazingira. Huenda wanajamii wakataka kuwasiliana na jamii nyingine ambako mwekezaji tayari anafanya shughuli kuulizia kuhusu uzoefu wao na mwekezaji huyo na jinsi ardhi yao, shughuli zao za kujikimu na maslahi yao mengine yalivyoathiriwa na mradi. Wanajamii wanaweza pia kutembelea miradi mingine ili kuona wao wenyewe jinsi mradi unaopendekezwa utakavyotekelezwa kiuhalisia.

# KUKAMILISHA MCHAKATO WA MASHAURIANO: KUAMUA KUKATAA UWEKEZAJI UNAOPENDEKEZWA AU KUFANYA MAELEWANO NA MWEKEZAJI

Baada ya kupitia upya taarifa zote muhimu kuhusu kampuni na uwekezaji unaopendekezwa, patahitajika majadiliano na wanajamii wote ili kufanya uamuzi kuhusu kuiruhusu au kuitoiruhusu kampuni hiyo kutekeleza mradi wake katika ardhi ya jamii. Wakati wa kufanya uamuzi huu, wanajamii wanapaswa kurejea na kufikiria kuhusu mambo yafuatayo:

- ➔ Mazoezi ya **kuainisha dira, thamani** na mpango kazi ulioibuliwa kutokana na mazoezi hayo;
- ➔ **Haki za jamii** chini ya sheria ya taifa na ya kimataifa;
- ➔ **Sheria ndogo ndogo za jamii, ikiwemo michakato ya ufanyaji wa maamuzi na mikakati ya kusuluhisha ugomvi iliyokubaliwa;**
- ➔ **Kuongezeka kwa utambuzi na uelewa** uliopatikana kwa kusoma nyaraka za mradi, kufanya utafiti kuhusu mwekezaji, na kuchambua athari zote chanya na hasi zinazoweza kutokea.

Punde jamii itakapokuwa imefanya uamuzi, inaweza kuitisha mkutano wa mwisho wa “mashauriano” na mwekezaji ili kutoa idhini au katazo kuhusu mradi.



Ili kusaidia kulinda maslahi ya jamii, andika vizuri kwenye karatasi maridhiano yao au kukataa kwao uwekezaji unaopendekezwa, na uambatanishe picha pamoja na video.

Katika kikao hiki, ambacho kinapaswa kuhudhuriwa na wanajamii wote, au wanajamii wengi iwezekanavyo, **jamii na watetezi wake wanapaswa kuandika kwa uangalifu ridhaa au katazo lao kwenye karatasi na kuambatanisha picha na video.**

Kuweka uamuzi wa jamii katika maandishi katalinda maslahi ya jamii na kuzuia madai batili kwamba jamii ilitoa ridhaa kwa hiari kabla ya mashauriano (wakati jamii ilikataa kutoa ridhaa).

Kabla mashauriano hayajakamilika, **wanajamii wanapaswa kudai wapewe nakala ya nyaraka zote muhimu;** mara nyingi jamii zinaachwa bila maandishi yoyote. Nakala zote za makubaliano katika maandishi zinapaswa kuhifadhiwa ndani ya jamii, na nakala iwekwe kwenye ofisi za serikali ngazi ya taifa na serikali za mitaa.

### ENDAPO JAMII ITAAMUA KUTOMRUHUSU MWEKEZAJI KUINGIA NA KUTUMIA ARDHI YAKE

Jamii ikiamua kwamba haitaki kampuni ijenge mradi wa uwekezaji kwenye ardhi yake, inaweza kuwa na haki ya kuamua kutotoa ardhi yake au kutoingia kwenye mkataba na mwekezaji mtarajiwa. Jamii inaweza kufanya hivyo kwa kutotoa ridhaa ya hiari kabla ya mradi, na inapaswa kuweka kumbukumbu ya uamuzi wa kutokukubali kwa maandishi. Kampuni na serikali zikikataa kukubali uamuzi wa jamii, watetezi na wanasheria wanaweza kuisaidia jamii kuendelea kuukataa mradi. Ikitokea hivyo, baadhi ya mikakati inayoweza kutumika ni pamoja na hii ifuatayo:

→ **Kuanzisha michakato inayotokana na nia njema:** Wakati mwingine, Tathmini ya Athari za Kimazingira, kesi zinazotokana na juhudi, na michakato mingine inayohitajika na serikali (au watoa mikopo wanaofadhili mradi wa uwekezaji) inatoa fursa kwa jamii kutoa madukuduku yake au kupinga matokeo, mipango, na mapendekezo. Watetezi wanaweza kuisaidia jamii kuchunguza ni michakato gani inafanyika na kuandaa mpango kwa ajili ya ushiriki wa wanajamii katika michakato hiyo ili watoe malalamiko yao au kupinga matokeo ya tathmini zilizofanyika.

→ **Kujihusisha na utaratibu wa usuluhishaji usiohusisha mahakama:** Kama ilivyojadiliwa hapo juu, jamii inaweza ikatumia sheria na vipimo vinavyohitajika na:

- **itifaki ya ndani ya kampuni;**
- **mifumo ya kimataifa ya uthibitishaji** kama vile mkutano uliowakusanya watu kujadili Mafuta ya Mawese Endelevu ambapo kila mmoja alichukuliwa kuwa na umuhimu sawa na mwingine;
- **taasisi zinazotoa mikopo na benki** zinazofadhili mradi;
- makampuni ya bima yanayokatia bima mradi;
- **wanaunuzi** wanaonunua bidhaa za kampuni; pamoja na
- **wakala na taasisi nyingine** zinaohusika na mradi pendekezwa.

kusaidia juhudi zao za kupinga mpango wa uwekezaji wa kampuni au uchukuaji wa ardhi kwa nguvu. Watetezi wanaweza kuwasaidia wanajamii kuchunguza ni vipimo gani vinaweza kutumika, iwapo kuna taratibu za usuluhishi zilizounganishwa na vipimo hivyo, na marekebisho yanayoweza kuwepo endapo jamii itapeleka malalamiko au kujiingiza katika taratibu za kutatua manung'uniko. Kama zipo taratibu za kutatua migogoro, jamii inaweza kuchagua kupeleka malalamiko kuzuia mradi.<sup>8</sup>

→ **Kampeni za utetezi:** Kampeni za utetezi zinazoeleza wasiwasi wa jamii kwa watendaji tofauti wa kitaifa na kimataifa zinaweza kusaidia kuinua uelewa kuhusu manung'uniko ya jamii na kuishinikiza serikali na kampuni kuangalia maslahi ya jamii. Wanajamii wanaweza kuhusisha vyombo vya habari kwa kueleza kinachowasibu kwa wanahabari, kuzungumza kwenye vipindi vya radio, kuandika makala na barua kwenye magazeti, na kuandika kwenye blogu mitandaoni. Kampeni ya jamii inaweza pia kunufaika ikiungana na mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo yanafanya shughuli zake kutumia kampeni ambayo yanaweza kusaidia kusambaza hali ya jamii na hadhira za kitaifa, kikanda na kiulimwengu. Jamii inaweza

<sup>8</sup> Huenda pakawa na taratibu za kushughulikia manung'uniko; kwa mfano, kama mwekezaji anatoka katika nchi ambayo ni mjumbe wa Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD), jamii inaweza kupeleka malalamiko kwa Mwakilishi wa Kitaifa wa OECD katika nchi anatokoka mwekezaji.



kutumia vyombo vya habari siyo tu kueleza nia mbaya ya kampuni, bali pia kuwaaibisha waliohusika katika mchakato mzima wa uwekezaji, yakiwemo mabenki yanayotoa fedha kwa kampuni, mashirika ya bima yanayotoa bima kwa shughuli za kampuni, wadau wa kampuni ambao wanaweza kushawisha maamuzi ya kampuni, na wadau wengine ambao wanaweza kuwa na ushawishi wa aina moja au nyingine. Aina hii ya utetezi unaweza kusaidia kuongeza shinikizo kwa kampuni kujibu masikitiko ya jamii.

⇒ **Kampeni za kushawishi:** Kampeni za kushawishi zinahusisha ufikiaji wa kimya kimya kwa serikali, wajumbe wa kampuni, taasisi na watendaji wengine wanaohusika kujaribu kuwashawishi wachukue hatua kusaidia nafasi ya jamii.

⇒ *Katika ngazi ya serikali za mitaa*, ambapo maafisa wa serikali wanaweza kuwa wako tayari zaidi kusikiliza mahitaji na matakwa ya wananchi wake, jamii zinaweza kuiomba serikali ya mitaa ipitishie sheria zinazozuia au kudhibiti baadhi ya biashara katika maeneo yao. Kutegemeana na sheria ya nchi, sheria hizo zinaweza *kuunganishwa na zoezi la serikali za mitaa la kuingiza vipengele vya kimahakama vinavyohusu usitawi*, ambavyo serikali inaweza kupitisha kulinda majimbo yao kutokana na uwekezaji unaoweza kuwa na madhara. Au, serikali za mitaa zinaweza pia kupitisha sheria inayowataka wawekezaji kufuata masharti kadhaa ili kampuni iweze kupata—na kuendelea kuwa na—kibali cha kufanya biashara kutoka kwa kitengo cha serikali za mitaa husika.

⇒ *Katika ngazi ya Serikali kuu*, jamii zinaweza kuwahusisha wawakilishi wao katika Bunge watumie nguvu zao za *“kusimamia mambo yote”* na kuiwajibisha Serikali (maafisa utawala wote) ifuate sheria za nchi zinazolinda mazingira na haki za jamii.

⇒ **Mkakati wa kufungua madai mahakamani:** Jamii inaweza pia kushauriana na mwanasheria na kuchagua kufungua shauri mahakamani dhidi ya mwekezaji na taasisi zote na watendaji wote wanaohusika. Kesi ya mahakamani inaweza kufunguliwa ili:

- ⇒ Kuimarisha au kutambua kwa uwazi zaidi haki za ardhi za jamii;
- ⇒ Kurejesha matumizi ya ardhi na jamii;
- ⇒ Kutambua rasmi haki ya jamii ya kutoa “Ridhaa Huru, Kabla, na iliyotokana na Uelewa wa jambo husika; au
- ⇒ Kupinga uhalali wa maamuzi ya serikali kutoa ruhusa kwa kampuni kutekeleza mradi (yakiwemo maamuzi ya serikali ya kutoa vibali, leseni, na kuidhinisha tathmini za athari, ripoti na mipango mingine).

⇒ **Vitendo vya moja kwa moja:** Vitendo vya moja kwa moja vinaweza kujumuisha maandamano, upingaji kauli za kushawishi watu wengine wagome, kuvamia makazi na kubakia papo hapo, migomo, na aina nyingine za uvunjaji wa sheria vilivyoandaliwa kwa ajili ya kutangaza manung’uniko ya jamii na, katika baadhi ya mazingira, kuzuia au kuchelewesha shughuli za kampuni. Kwa usalama wa jamii, juhudi za moja kwa moja zinapaswa zisiwe za kikatili. Juhudi za moja kwa moja zinatakiwa zichukuliwe tu kama njia ya mwisho, kwani zinaweza kuchukuliwa kama uvunjaji wa sheria, na hivyo kusababisha hatari kwa wanajamii, ikiwemo kufungwa, kufunguliwa kesi za jinai, na uonevu au ukatili unaoweza kufanywa na askari wa ulinzi.

Kwa mikakati yote hii inayoweza kutumika, wanajamii wanatakiwa kutafuta ushauri wa kisheria na kitaalamu kuhakikisha kwamba wanaelewa matokeo ya juhudi zao za kupinga uwekezaji. Kutegemeana na muktadha, baadhi ya mikakati inaweza kusababisha hatari kubwa kwa wanajamii. Kwa mfano, kuzungumza dhidi ya mradi huku wakisaidiwa na watu wenye nafasi katika jamii kunaweza kuwaweka wanajamii katika hali ya hatari kimwili au kuwa hatarini kufungwa.

## IWAPO JAMII ITAAMUA KUMWACHIA MWEKEZAJI ATUMIE ARDHI YAKE

Iwapo jamii itaamua kugawa ardhi yake na mwekezaji mtarajiwa, uamuzi huu utakamilisha mchakato wa mashauriano kwa kuonesha kukubali kuafikiana masharti ambayo yatazingatiwa uwekezaji ukiendelea. Cha muhimu zaidi kukumbuka ni kwamba, kuingia katika mchakato wa mashauriano hakumaanishi kwamba jamii ime: (1) ahidi kwamba mkataba utafikiwa, au (2) toa ruhusa kwa mwekezaji kutumia ardhi ya jamii.

Kwasababu hii ni awamu mpya yenye taratibu mpya, jamii inaweza ikahitaji msaada tofauti au watu wenye uzoefu mkubwa zaidi kisheria na kitaalamu, pamoja na ufadhili mpya na rasilimali za ziada kwa ajili ya mchakato rasmi wa mashauriano.

### MASHAURIANO NI NINI?

Majadiliano ya mashauriano yanahusisha watu wawili au pande mbili au zaidi ambazo zinakaa pamoja kufikia makubaliano kuhusu masharti halisi ya namna watakavyofanya kazi pamoja, kuwasiliana, au kubadilishana au kugawana rasilimali. Katika mchakato wa mashauriano, jamii na mwekezaji wanakuja mezani na matarajio yao mahususi na kujadili mpaka wafikie mwafaka ambao pande zote mbili zinakubaliana nao.

Jamii haipaswi kukubali au kukataa kile mwekezaji anachoahidi kama mkataba kamili ambao ni lazima waukubali au waukatae kama ulivyo. Badala yake, mkataba wa maridhiano utahusisha majadiliano na miafaka itakayojumuisha masuala mbalimbali, ambayo yataandikwa kwa muhtasari kama vipengele tofauti vya mkataba. Wakati wa mashauriano, mwekezaji na jamii wanaweza kutoa ahadi na kubadilisha ahadi hiyo na kutoa ahadi nyingine, kila upande ukishinikiza masharti ambayo yataunufaisha zaidi na kulinda maslahi yake.

*Kwa kila kipengele cha mkataba, timu ya mashauriano ya jamii haitakiwi ijihisi kwamba inaharakishwa kufanya maamuzi. Badala yake, timu ya mashauriano ya jamii inapaswa kuuliza maswali ili kuhakikisha inaelewa vizuri kile kinachoahidiwa, na kisha kuchambua ahadi hizo kwa makini huku wakishauriana na mwanasheria, msaidizi wa kisheria, au mtetezi wao kabla ya kutoa ahadi mbadala au kukubali masharti yanayotolewa na mwekezaji. Hii ndiyo sababu, kuingia katika mashauriano, wanajamii ni lazima wafahamu kile wanachotaka, ikiwemo kile ambacho wako tayari kuridhia (kwa mfano, kodi halisi ya mwezi ambayo italipwa kwa jamii) na kile ambacho hawako tayari kuridhia (kwa mfano, ulinzi unaolinda maeneo muhimu kwa jamii na mfumo wa upatikaji maji) tazama Mwongozo 2 kujifunza zaidi kuhusu mambo ya kuzingatia wakati wa mashauriano kwa ajili ya mkataba).*

# KUJIANDAA KWA AJILI YA KUAFIKIANA KUHUSU MKATABA KATI YA JAMII NA MWEKEZAJI

Endapo jamii itaamua kushauriana na mwekezaji, wanajamii na watetezi na wanasheria wao wanapaswa kuanza mara moja kujiandaa kwa ajili ya mashauriano. Maandalizi hayo ni pamoja na kuunda timu ya mashauriano na kuamua namna timu hiyo itakavyokuwa inatoa taarifa na kuishirikisha jamii; kukubaliana na mwekezaji kuhusu muundo wa mashauriano; na kupitia au kuainisha mipango na vipaumbele kabla ya kuingia katika mashauriano. Maandalizi haya yameelezwa katika kurasa zinazofuata.



Ikiwa jamii itakubali kuchangia ardhi na rasilimali zao na mwekezaji, **isiuze ardhi yao kamwe**. Mkataba wa kukodisha utahakikisha kwamba ardhi inabaki chini ya umiliki wa jamii na itarudishwa kwa jamii uwekezaji unapofikia ukomo.



Teua kikundi cha wanajamii wenye sifa na ujuzi tofauti wanaoheshimika ndani ya jamii washirikiane na watetezi na katika mashauriano ya kuingia mkataba na mwekezaji mtarajiwa.



## KUUNDA TIMU YA MASHAURIANO ITAKAYOIWAKILISHA JAMII NA KUANDAA MPANGO WA MAWASILIANO

Jamii inapaswa kuamua ni nani atakaeiwakilisha wakati wa kukutana na wawakilishi wa kampuni. Pamoja na yote, jamii inapaswa kuweka vigezo vya ulinzi ili kuhakikisha hakuna mtu alieidhinishwa kuamua kwa niaba ya jamii, hususan kufikia mwafaka, kukata shauri, kuingia katika upatanisho au maamuzi, na kutia saina maandishi rasmi ya utetezi yaliyoandikishwa mahakamani, **ili kuzuia uwezekano wa kutolewa rushwa na hongo, inatakiwa pawepo na angalau watu watatu (ikiwezekana zaidi) ambao kwa pamoja watakutana na mwekezaji kuwakilisha maslahi ya jamii na kutia saina nyaraka zozote ambazo zitaifunga jamii.** Ili kuchagua watu sahihi kwa kazi hii, jamii inapaswa kuitisha mkutano mkuu na kujadilia yafuatayo:

- Je, viongozi wa jamii, viongozi walioteulwa, au “timu ya mashauriano” iliyoundwa yenye wajumbe wanaume, wanawake, vijana na wazee waliochaguliwa mahususi kwa ajili ya shughuli hii, wataiwakilisha jamii?
- Ni kwa namna gani timu ya mashauriano inaweza kuwakilisha matakwa na maslahi ya vikundi vyote vya wadau katika jamii, ili maoni ya wanajamii wote yaweze kuzingatiwa?
- Wajumbe wa timu hii wanapaswa kuwa na sifa zipi? (Kwa mfano, akili au uwezo wa kufikiri, uaminifu, uadilifu, wenye kuaminika, utulivu, ujasiri, heshima, na uwezo wa kusikiliza, n.k.)
- Je, wajumbe wa timu hii wanapaswa kuwa na ujuzi gani? (Kwa mfano, uwezo wa kusoma na kuelewa, uwezo wa kuzungumza lugha ya taifa au lugha ya wawekezaji, uzoefu wa kufanya kazi na viongozi wa serikali, uwezo wa kuzingatia utamaduni wa jamii na wa mwekezaji, umahiri katika kuwasilisha na kutetea wazo/kuzungumza mbele za watu, n.k.)

PATA  
USHAURI  
WA KISHERIA

Ikiwezekana, ni vyema kuwa na mwanasheria au msaidizi wakisheria anaeaminika kwenye timu ya mashauriano au anaeishauri kwa karibu timu hiyo.

Jamii inapaswa kuainisha wajibu na majukumu ambayo kila mjumbe wa timu ya mashauriano atakuwa nayo. Pamoja na kuhakikisha kwamba mawazo ya wanawake, vijana, na watu kutoka katika makundi vyenye watu wachache yanawakilishwa, timu ya mashauriano inatakiwa iwe na wajumbe ambao wanaweza kufanya yafuatayo:

- Kuongoza mashauriano kwa niaba ya jamii, huku wakiweka maslahi ya jamii moyoni hata pale mwekezaji anapojaribu kuyasukuma kando;
- Kuwasiliana na kuzungumza vizuri;
- Kuandika dondoo ambazo zinawekwa katika kumbukumbu ya maandishi yote yale yanayojadiliwa na kuamuliwa katika mikutano vyote na maafisa wa kampuni;
- Kuomba ufafanuzi kwa kujiamini pale ambapo jambo lolote linakuwa haliko wazi;
- Kuwaweka watu wote katika mstari, wakizingatia muda, na wakijipanga vyema;
- Kuongoza mikutano vizuri, ikiwemo kusaidia kusimamia tofauti zinazojitokeza katika timu na kuiweka timu katika hali ya umoja; na
- Kufanya shughuli zozote nyingine ambazo jamii inaziona ni muhimu wakati wa kushauriana kwa niaba yao.

Ili kuhakikisha kwamba timu ya mashauriano inawajibika kwa jamii wakati wote, **jamii inapaswa pia kuainisha vile ambavyo timu ya mashauriano na jamii watawasiliana**, ikiwemo kujadili, kuamua, na kukubaliana kuhusu yafuatayo:

- Jinsi ambavyo jamii itahakikisha kwamba matakwa ya kila mmoja yanawakilishwa na timu ya mashauriano.
- Mambo ambayo timu ya mashauriano inaweza kuamua pekee yake na mambo ambayo ni lazima wayalete kwenye jamii ili yajadiliwe na jamii nzima na kuamuliwa kwa pamoja
- Mara ngapi na kwa njia gani, timu ya mashauriano itoe mrejesho kwa wanajamii kuhusu maendeleo ya mashauriano na kuomba mawazo yao? (Wakati wa mchakato wa mashauriano, kutakuwa na mikutano ya kila siku au kila wiki?)
- Ni maamuzi gani, wakati wa mashauriano ambayo timu ya mashauriano inaweza kufanya bila kushauriana na jamii nzima?

→ Ni maamuzi gani ambayo yanahitaji ridhaa na makubaliano ya jamii nzima?

→ Je, timu ya mashauriano inaweza kuvuka au kwenda mbali zaidi ya masharti ambayo jamii imekubaliana kama “mipaka” ya juu au chini ya yale ambayo jamii inakubali kufikia mwafaka?

Michakato ya aina hii inaweza kutumika na jamii kubwa ili kuiweka timu ya mashauriano kwenye mstari na iwajibike wakati wote wa mchakato wa mashauriano.

Baada ya timu ya mashauriano kuchaguliwa, watetezi wanaweza kuwasaidia wajumbe wa timu hii kutimiza majukumu yao kwa **kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo**. Mafunzo hayo yanaweza kujumuisha mambo yafuatayo:

- Maandalizi kwa ajili ya mazingira yanayoweza kujitokeza wakati wa mashauriano, ikiwemo kuandika dondoo za mambo ya kuzungumza na kupanga namna ya kuwasilisha utetezi dhidi ya masharti ambayo mwekezaji anaweza kuweka ambayo yanaweza kuiumiza jamii;
- Maigizo yanayoonesha mchakato wa mashauriano unavyokuwa (huku timu ya mashauriano ikicheza nafasi ya timu ya mashauriano, na wanajamii au watetezi wakicheza nafasi ya wawekezaji);
- Uandaaji wa maneno ya kuzungumza kabla mashauriano hayajaanza ambayo yanaainisha malengo na wasiwasi wa jamii;
- Uandaaji wa mpango wa utendaji na ratiba ambayo inajumuisha maandilizi yote muhimu hadi kufikia muda wa mashauriano, na kupangiana majukumu na wajibu ili kuhakikisha taarifa zote muhimu zinakusanywa, mikutano yote muhimu ya jamii inaitishwa, na utaratibu wa ugavi wa vitu na watu umeshughulikiwa; na
- Utoaji wa mafunzo na mazoezi ya kujenga ujuzi ambayo yanaweza kusaidia kuiandaa timu ya mashauriano iwakilishe vizuri maslahi ya jamii.

## **KUKUBALIANA KUHUSU MCHAKATO, MAHALI, MUDA NA LUGHA YA MASHAURIANO**

Kabla mashauriano hayajaanza, viongozi wa jamii na/au timu ya mashauriano iliyochaguliwa wanapaswa wakutane na mwekezaji (na maafisa wa serikali husika, kama ikibidi) na kukubaliana kuhusu kanuni za jinsi mashauriano yatakavyokwenda.

→ **Nani atafanya mashauriano kwa niaba ya pande zote na jinsi watakavyotambuliwa?** Jamii itaitambulisha timu ya mashauriano kwa mwekezaji, na kupata majina na vyeo vya watu watakaomwakilisha mwekezaji (huenda ikawa ni timu ya kisheria ya mwekezaji).

→ **Mwekezaji na jamii watawasiliana vipi kuhusu ugavi wa vifaa na watu wakati wa mashauriano?** Nani kutoka katika jamii ataidhinishwa kuzungumza na mwekezaji au mawakala wake kuhusu masuala ya upangaji wa ratiba na masuala mengine ya kiutendaji yanayohusiana na mchakato wa mashauriano, nje ya makubaliano halisi ya mkataba? Endapo jamii itahitaji kumpigia mwekezaji ili kuwasiliana, watumia namba gani na watazungumza na nani?

→ **Mashauriano yatachukua muda gani mpaka yakamilike?** Mashauriano yataanza wakati gani? Yanapaswa kumalizika wakati gani?

→ **Kutakuwa na mikutano mingapi ya mashauriano?** Wanajamii wanapaswa kudai kwamba pawepo na kikao zaidi ya kimoja cha mashauriano, ili kuruhusu timu ya mashauriano kutoa mrejesho kwa jamii kubwa kuhusu jinsi mashauriano yanavyokwenda, kujadili mapendekezo ya kampuni ya uwekezaji, kufanya utafiti unaohitajika, pamoja na kufanya maamuzi kuhusu majibu na masharti mbadala ya jamii.

→ **Mashauriano yatafanyika wapi?** Sehemu mashauriano yanapofanyika inaweza kuathiri uwiano wa nguvu wakati wa mashauriano: kama mikutano itafanyika katika ofisi za kampuni jijini, timu ya mashauriano ya jamii inaweza ikaogofya. Badala yake, mashauriano yanapaswa yafanyike mahali ambapo panafikika kirahisi na wanajamii, katika sehemu ambayo watajisikia huru. Ni vyema kukubaliana kuhusu mahali pasipopendelea upande wowote, kwa mfano ndani ya au karibu na jamii ili wanajamii waweze kuhudhuria na kutazama kwa urahisi.

→ **Mashauriano yataendeshwa kwa lugha gani?** Kwa kawaida, mashauriano yanapaswa kuendeshwa katika lugha inayotumika na jamii husika huku pakiwa na wakalimani kwa ajili ya mwekezaji. Endapo mwekezaji atadai kwamba mikutano ifanyike kwa lugha ya kiingereza au lugha ya taifa, hakikisha kwamba: (1) wakalimani

wanafahamu vizuri lugha zote mbili za mashauriano pamoja na lugha inayotumika katika jamii (2) wanao uwezo wa kutafsiri kile kinachosemwa kwa lugha nyepesi na wazi ili wawakilishi wote wa jamii waliopo katika mashauriano waweze kuelewa.

Punde mambo hayo yote yakikubalika, **masuala haya yanapaswa kuandikwa katika mpango wa mashauriano** ambao unaweza kutumika kama rejea wakati wote wa mchakato wa mashauriano.

### **KUPITIA UPYA VIPAUMBELE VYA JAMII, KUELEWA NI NINI MWEKEZAJI ANATAKA, NA KUANDAA KWA AJILI YA MWAFKA**

Kabla mashauriano hayajaanza, wanajamii wanapaswa kupitia juhudi za maandalizi yao ya awali (zimeelezwa katika sehemu 1, hapo juu), zikiwemo:

- Kupitia upya dira ya jamii ya siku za usoni na mpango wa matumizi ya ardhi unaoendana na dira hiyo;
- Kukumbuka ni thamani kiasi gani ambayo wao wenyewe wanapata kutoka katika ardhi na rasilimali zao;
- Kupitia upya sheria ndogo ndogo za jamii, zikiwemo mpango wake wa kushughulikia matatizo ya kutoelewana wenyewe kwa wenyewe au ugomvi kati ya wanajamii unaotokea wakati wa mashauriano;
- Kupitia upya matokeo ya tathmini za athari ili kuhakikisha kwamba maeneo yote yanayohitaji ulinzi yameingizwa katika mkataba; na
- Kupitia upya sheria za taifa, zikiwemo:
  - Sheria za kitaifa na kimataifa zinazohitaji mwekezaji azifuate;
  - Kufahamu kama serikali imekwisha tia saina mkataba na mwekezaji, na kama hivyo ndivyo, kufahamu masharti ya mkataba.

Muhimu zaidi, jamii inapaswa **kujiandaa kuisitiza baadhi ya masuala na kuafikiana kuhusu mengine.**

Mambo ambayo jamii iko tayari kuafikiana (kwa kiasi gani), na mambo gani ambayo hayawezi kubadilika (non-negotiable), yanapaswa kupitiwa upya na kuwekwa wazi, ili mamlaka walio nayo wajumbe wa timu ya mashauriano yawe wazi na yajulikane.

**Jamii inapaswa kuhakikisha kwamba inaelewa kile ambacho mwekezaji anataka na kwanini.**

Wanajamii wanapaswa kuhakikisha kwamba wanaelewa malengo ya mwekezaji ni nini, kwani taarifa hii itaisaidia timu inayofanya mashauriano kuelewa nini kinawezekana wanapokuwa katika mashauriano na itawaweka katika nafasi imara zaidi wakati wa maridhiano. Wawekezaji wanaweza kujaribu kuficha maslahi yao, kiwango cha mwisho ambacho wako tayari kulipa, au faida ya ardhi na rasilimali wanazotaka. Wanajamii na watetezi wanapaswa kupitia nyaraka zote za mwekezaji ili kuelewa vizuri zaidi maslahi, nia na uwezo wake na hivyo wawe tayari kujibizana vizuri kile ambacho mwekezaji atajaribu kupata.

**Mwisho, jamii inapaswa kufikiria na kupanga kwa ajili ya kile kinachoweza kutokea endapo jamii na mwekezaji hawataafikiana.**

Kama jamii haijisisikii vizuri kuhusu kile mwekezaji anachotoa na mwekezaji hayuko tayari kufikia maridhiano, jamii inaweza kuamua kufunga mchakato wa mashauriano na kukataa mradi unaopendekezwa. Hata hivyo, ni lazima jamii ielewe na kufikiria kuhusu madhara ya kufunga mashauriano: kama ridhaa ya jamii inahitajika kulingana na sheria ya nchi, basi mradi unaweza usiruhusiwe kuendelea. Hata hivyo, kama sheria ya nchi—au watendaji wa kitaifa wenye mamlaka—inaweza kuruhusu uwekezaji uendeleo hata bila ridhaa ya jamii, basi kufunga mashauriano bila kuwa na mkataba wa maandishi ulio wazi, kunaweza kuiweka jamii katika hali mbaya zaidi.



## KUANZA MASHAURIANO

Kama jamii imekubali kugawana ardhi na maliasili zake na mwekezaji mtarajiwa, basi mchakato wa mashauriano ili kupata mkataba unaofunga pande zote ambao una faida kwa jamii na kwa mwekezaji yataanza. Jamii zinazolingia katika mashauriano zinapaswa kuwa makini kuhusu ukosefu wa uwiano wa nguvu na taarifa, na kadri inavyowezekana, zitafute msaada na ushauri wa wanasheria wasaidizi, wakisheria, wataalamu, na watetezi wengine. Juhudi zinapaswa zifanyike kuhakikisha kwamba mkataba unaandikwa kwa kutumia lugha ya kawaida, nyepesi ambayo inaeleweka kwa wanajamii (ambao lazima wafuate masharti ya mkataba) na maafisa wa serikali (ambao wanaweza kulazimika kusimamia utekelezaji wa masharti ya mkataba).

Mwongozo 2 kinatoa mwongozo kwa jamii zinazojiandaa kwa ajili ya mashauriano na kuandaa mikataba na wawekezaji watarajiwa. Kinaanza kwa kuelezea mkataba ni nini na kueleza aina tofauti za mikataba ambayo jamii na wawekezaji wanatia saina. Kisha kinaelezea vitu gani vinavyoweza kuingizwa katika mkataba na kutoa mapendekezo na kuzikumbusha jamii kuhusu mambo muhimu wanayopaswa kuyaingiza katika mkataba wowote ambao wanatia saina. Ili kuzisaidia jamii ziamue nini watetee katika mikataba wanayoafikiana, kila sehemu inaorodhesha maswali ambayo wanajamii wanaweza kuyajibu wakati wanapojiandaa kwa ajili ya kushiriki katika mashauriano.

Wakati wa mashauriano kuhusu masharti ya kumpa mwekezaji mtarajiwa, kuweni makini kuhusu ukosefu wa uwiano katika nguvu ya maamuzi na upatikanaji wa taarifa, ulizeni maswali mengi, na musisitize kwamba maswali yenu yajibiwe.





MAANDALIZI

KABLA WAWEKEZAJI  
WATARAJIWA  
HAWAJAFIKA



Kituo cha Uwekezaji Endelevu cha Columbia ni kituo kinachoongoza kwa utafiti unaotumika, na jukwaa lililoundwa kwa ajili ya kujifunza, kujadili na uwekezaji endelevu wa kimataifa.

[ccsi.columbia.edu](http://ccsi.columbia.edu)



Namati ni shirika la kimataifa lililoundwa kwa ajili ya kuendeleza nyanja ya uwezesaji wa kisheria na kuimarisha uwezo wa watu wa kudai na kulinda haki zao.

[namati.org](http://namati.org)

*“Miongozo hii inavyohitajika sana kuziba pengo muhimu: ni pale tu jamii zinapowezeshwa ndipo zinapoweza kufanya **chaguzi huru, zinazotokana na uelewa** na kujenga ubia **wenye tija (manufaa)** na serikali na sekta binafsi.”*

- LORENZO COTULA, IIED

